**Bunge** laridhia mapendekezo ya TPA na DPW ufanisi bandari
UKURASA 3



**Maandamano** ya wafanyabiashara yatikisa kupinga malori kuzuiwa
UKURASA 2



Ukurasa 12
MIAKA 60 AFRIKA
**Ni kama hakuna tena matumaini kumejaa hofu, vita na kukata tamaa**

Ukurasa 13
BAHARI YACHAFUKA TLP
Mwenyekiti wa Vijana Vs Katibu Mkuu, uchaguzi sasa ni ndoto

siasa
JUMATANO JUNI 7, 2023
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU

Ukurasa 14
**RECEP TAYYIP ERDOGAN: 'Dikteta' aliyeshinda kwenye marudio ya uchaguzi Uturuki**

KADA ALI KARUME
**Anyooshewa kidole, Mwinyi aelekeza wavunja miiko CCM washughulikiwe**
• Hofu ni kuepuka yaliyowahi kutokea zamani

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

MVUTANO unanukia katika siasa za visiwani, huku hatima ya Balozi Ali Karume, mtoto wa mwasisi wa Serikali ya Mapinduzi (SMZ), Sheikh Abeid Amani Karume, akiibua mshangao baada ya kuzusha hoja zenye masuala mengi yenye utata.

Mjadala unaoibuliwa na Ali Karume, unasababisha mvutano wa maneno kwa makada wa chama wengine wakitaka aitwe na Kamati ya Maadili ya CCM kuhojiwa, kuhusu madai kuwa haijashinda chaguzi za vyama vingi kutokana na kusimamisha wagombea ambao si chaguo la wana CCM.

Balozi Karume anawaambia waandishi wa habari visiwani hapa nyumbani kwake Maisara hivi karibuni kuwa CCM imekua ikiteua mgombea badala ya kuchaguliwa na wanachama jambo ambalo linadumaza ...

"Wagombea watano walipelekwa Kamati Kuu badala ya kujadaliwa na Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya Zanzibar iliwapendekeza Dk. Khalid Salum Muhammed, Shamsi Vuai Nahodha, Profesa Makame Mbarawa, Khamis Mussa na Dk. Hussen Ali Mwinyi," anasema.

Anaongeza kuwa majina hayo yalichunjwa na kubakia matatu katika kikao halali cha Kamati Kuu na ndiyo yaliyopigiwa kura ya wazi akiwamo Dk. Khalid Salum, Shamsi Vuai Nahodha na Dk. Hussein Ali Mwinyi na wajumbe wa Halmashauri Kuu Taifa ya chama hicho.

Mbeto anamwambia Karume kuwa kwa mujibu wa miiko na maadili ya CCM, mwanachama yeyote kama ana jambo lake anapaswa kuliwasilisha katika ...

UKURASA 11

# Nipashe

Jumatano Juni 7, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com
ISSN 0856 • Na. 0581334

The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



Watumishi wa Mfumo wa Maeneo Tengefu Dar es Salaam (DMRS) chini ya Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengufu (MPRU) na wadau mbalimbali wakifanya usafi katika ufukwe wa Kisiwa cha Bongoyo, Dar es Salaam, kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani juzi. **Picha ndogo:** Baadhi ya sindano zilizookotwa ufukweni mwa bahari. **PICHA: MPRU**

# Sindano zilizotumika zinavyotupwa baharini



• **Taka** za plastiki nazo zabainika... *Endelea ukurasa wa 2*




Moja ya mabehewa sita ya treni ya abiria yaliyokarabatiwa nchini Uturuki kwa ajili ya kutumika katika reli ya kisasa (SGR) yalipowasili Bandari ya Dar es Salaam jana. **PICHA: JAMES KANDOYA**

## Mabehewa ya ghorofa SGR yatua

UKURASA 2

RIPOTI YA UCHUNGUZI-3
MZEE PHABIAN HEVORD

## Babu, muuguzi mstaafu aliyegeuka gwiji mpekuataka Pugu Kinyamwezi

• **Umaarufu** wake; msomi pekee katika dampo... *Ukurasa 4*

MICHEZO KWA MKAPA MICHEZO YA KIMATAIFA TU UK.23 KATUNI UK.6

# Sindano zilizotumika zinavyotupwa baharini

**Na Romana Mallya**

MABOMBA ya sindano na plastiki ni moja ya taka ngumu zilizookotwa kwa tani katika visiwa na fukwe za Bahari ya Hindi, hali inayotishia usalama wa watu na viumbe hai.

Meneja wa Kitengo cha Hifadhi za Habari na Maeneo Tengefu (MPRU), Dk. Immaculate Semesi, alibainisha hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu Maadhimisho ya Siku ya Bahari Duniani yanayofanyika Juni 8, kila mwaka.

Alisema katika maadhimisho ya mwaka huu ambayo yamebebwa kaulimbiu isemayo 'Sayari ya Bahari na Mawimbi Yanayobadilika', mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango.

"Kwa miaka 10 iliyopita, siku maalum ama ya Mazingira Duniani au Siku ya Bahari Duniani wakati wa kusafisha fukwe umekuwa ugonjwa sugu kwenye fukwe tunakokwenda kusafisha tunakutana na taka za kila aina.

"Taka ngumu ikiongozwa na plastiki ikiwa namba moja, chupa za aina nyingi, mifuko na sasa hivi mpaka zile syringes (mabomba ya sindano ya hospitali) tunaziokota si tu kwenye fukwe huku nchi kavu, lakini pia kwenye visiwa vyetu tunaokota tani kadhaa," alisema Dk. Semesi.

Alisema Juni 5, ambayo huwa Siku ya Mazingira Duniani waliposhiriki kwenye usafi uliofanyika kwenye visiwa na miongoni mwa taka walizokutana nazo.

Alisema wameona kuna shida ya kuratibu taka zinazozalishwa nchi kavu kwenye viwanda, majumbani na mashambani zikihusisha taka ngumu na za vimiminika.

Kutokana na uharibifu huo, alisema wanataka kuirejesha bahari kwa kuithaminisha vile inavyotakiwa.

"Uharibifu mazingira wa bahari pia hutokana na uvunaji wa rasilimali ya mazao baharini namba moja tunavuna kupitiliza mpaka wale vitoto. Namba mbili ni matumizi ya zana zisizo sawa na kwa sasa kumetokea matumizi ya uvuvi wa mabomu ambao miaka kama sita ulishamiri na kupungua na sasa umerudi tena," alisema.

Pia alisema suala lingine ni vyombo vya usafiri baharini zikiwamo feri, meli za mizigo zinazosafirisha mafuta, wakati mwingine vimekuwa vikichafua mazingira ya bahari na wakati mwingine kutoa sauti ambazo huathiri viumbe.

"Ukiharibu hali ya joto la bahari unaharibu mzunguko wa maji baharini na kwa sasa kwa asilimia kubwa ya maji yetu duniani inaelekea ICU (Chumba cha Uangalizi Maalum) ndio maana lazima tuchukue hatua za haraka kama nchi zote duniani," alisema.

Mtaalamu huyo alisema kupitia mkutano huo wamewaalika watoa uamuzi ngazi ya siasa, serikali, watendaji na jamii, ili waweze kutoka na muafaka ambao utawawekea malengo na mikakati mahususi ya kutibu bahari na kuihifadhi.

Alisema duniani wamekubaliana nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa (UN) kwamba ifikapo mwaka 2030, angalau asilimia 30 ya bahari duniani iwe imehifadhiwa na kwa sasa wako chini ya asilimia tatu na Tanzania Bara imehifadhi asilimia 6.5 tu.

Kutokana na hali ya bahari, alisema utumiaji wake unakwenda ukibadilika ndiyo maana wakiwa wasimamizi wakuu wa rasilimali za bahari nchini, wameamua kuandaa mkutano maalum ukihusisha viongozi wa ngazi ya juu. Dk. Mpango ambaye ndiye anayesimamia masuala ya mazingira.

"Bahari imekuwa ikipata changamoto za kimazingira kwa kasi kubwa nchini na duniani. Jukumu letu mahususi ni kusimamia na kuhifadhi rasilimali bahari, tunasimamia eneo la kilometa za mraba 2,000 tunasimamia maeneo ya hifadhi Tanga, Mafia, Mtwara na Dar es Salaam," alisema.

Mhifadhi Mkuu MPRU, Godfrey Ngupula, alisema kwa sasa Dar es Salaam mvua zikinyesha watu ndio wanafungulia vyoo na uchafu wote unaingia baharini na kuharibu uwiano wa ikolojia na kusababisha uzalianaji hauendelei.

"Maendeleo ya uchumi tuliyonayo kila mtu akitaka kujenga atakwambia anataka viwanja vya ufukweni ndio maana vinauzwa ghali.

"Unapojenga kule wakati mwingine ndio unaanza kuharibu kama kasa wanakimbilia kutaga kule, maana yake shughuli nyingine zinakuwa zimeingilia, uharibifu unatokea matokeo yake tunaona samaki hatuwezi kuwapata," alisema.

Mkuu wa Kitengo cha Mipango wa MPRU, Andulile Mwaisaka, alisema wanataka wananchi waione bahari kama msambazaji namba moja wa huduma zote za kiuchumi na kijamii.

"Uchumi wetu unaendeshwa kwa asilimia 80 na bahari tukiitumia vibaya tutafika mahali hakuna chakula na taifa litakosa mapato ya rasilimali samaki," alisema.



Kaimu Meneja wa Elimu kwa Mlipakodi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Hamad Mterry (kushoto), akizungumza wakati wa semina kwa waandishi wa habari kuhusu kuongeza uelewa wa masuala ya kodi za ndani na forodha jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MASALA**

# Mabehewa ya ghorofa SGR yawasili

**Na Romana Mallya**

MABEHEWA sita ya ghorofa yaliyokarabatiwa kati ya 30 yatakayotumika kwenye mradi wa Reli ya Kisasa (SGR) yamewasili nchini.

Mabehewa hayo yametengenezwa na Kampuni ya Lueckermeier Transport and Logistic GMBH ya Ujerumani.

Mkuu wa Uhusiano wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Jamila Mbarouk, alisema jana kuwa mabehewa hayo tayari yameshawasili katika Bandari ya Dar es Salaam na utaratibu wa kuyapokea unafanyika.

"Ni kweli mabehewa sita yaliyokarabatiwa yameshawasili ni yale ya ghorofa, tunafanya utaratibu wa kuyapokea na unaweza kufanyika kesho kutwa (Alhamisi)," alisema na kuongeza kuwa mabehewa mengine saba kama hayo yanatarajia kupokelewa Agosti, mwaka huu na mengine yatawasili kwa awamu.

Mei 31, mwaka huu, Mkurugenzi wa Idara ya Habari Maelezo na Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, alisema baada ya kupokea mabehewa 14 kati ya 59 kutoka kampuni ya Hyundai Rotem ya Korea Oktoba, mwaka jana, na mabehewa hayo sita kati ya 30, yatawezesha kuanza kwa shughuli za uendeshaji haraka kama ilivyotarajiwa.

Msigwa alisema alipokuwa akitoa ufafanuzi kuhusu kuchelewa kuanza utoaji wa huduma za usafiri wa reli kwa kutumia treni ya SGR Mei, mwaka huu, kama ilivyotarajiwa.

Alisema kuchelewa kuanza kwa huduma hiyo kulitokana na kutokukamilika kwa matengenezo ya vichwa viwili vya kuvutia treni kwa wakati, hivyo kusababisha majaribio ambayo yalitarajiwa kuanza mwezi uliopita kusogezwa mpaka mwezi ujao.

"Hatuwezi kuendesha treni bila vichwa. Baada ya kuvunjika mkataba kati ya TRC na Eurowagon ya Uturuki, mkataba wa matengenezo ulihamishiwa Lueckermeier Transport and Logistic GMBH ya Ujerumani.

"Kumekuwa na changamoto ya utengenezaji wa vichwa kutokana na shida ya upatikanaji wa vipuri vinavyotumika katika ukamilishaji wa vichwa vya treni kwa sababu ya ugonjwa wa UVIKO -19 na vita vya Russia na Ukraine vimesababisha kuharibika kwa uchumi duniani. Hizo ni sababu za msingi zilizofanya ucheleweshaji huo," alisema Msigwa.

Alisema kichwa cha kwanza cha treni kati ya viwili vinavyotengenezwa nchini Ujerumani na kampuni ya Lueckermeier Transport and Logistic GMBH kitawasili mwezi ujao, hivyo kuwezesha majaribio ya treni hizo kuanza.

## Madereva, wafanyabiashara waandamana malori kuzuiwa

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

MADEREVA na wafanyabiashara wanaotumia mpaka wa Tanzania na Malawi eneo la Kasumulu wilayani Kyela mkoani Mbeya, wameandamana kushinikiza viongozi wa serikali za nchi hizo kukubaliana kuondoa baadhi ya tozo ambazo zinawaumiza katika utekelezaji wa majukumu yao.

Maandamano hayo yametokana na kushikiliwa kwa magari zaidi ya 300 katika maeneo mbalimbali ya Malawi huku 100 yakiwa mita chache kutoka eneo la mpaka, wamiliki wake wakitakiwa kulipa tozo inayotozwa na Mamlaka ya Mapato Malawi (MRA).

Akizungumza jana katika mpaka wa Kasumulu, mfanyabiashara wa mazao nchini, John Mwakipesile alisema tangu Mei 17, madereva wa malori walizuiwa Malawi, jambo ambalo siyo sahihi kwa kuwa muda wa kuanza kwa sheria hiyo ulikuwa haujawadia.

Alisema moja ya sababu zinazodaiwa madereva hao kuzuiwa ni kutolipa kodi mpya ya usafirishaji ambayo ilianza kutumika Mei 18 na kwamba walishaanza safari Mei 16 na kukaribia eneo la mpaka Mei 17, mwaka huu, lakini walitakiwa kulipia, jambo ambalo wanaona haliko sawa.

"Hadi sasa magari yetu ambayo yamebeba bidhaa mbalimbali zimeharibika, tumepata hasara kubwa sana maana bado tunaendelea kuwalipa madereva wetu na tozo nyingine za barabarani," alisema Mwakipesile.

Jacob Mwakalobo, mfanyabiashara, alisema mazingira ya kufanya biashara yamekuwa magumu kwao kutokana na wingi wa kodi Malawi,

mmoja wa madereva ambao magari yao yalizuiwa Malawi, Anthony Nelson alisema walishi maisha magumu baada ya kuzuiwa eneo la Kambi ya Jeshi ambalo upatikanaji wa baadhi ya huduma ulikuwa mgumu.

Joseph Anyangalile, mfanyabiashara mpakani Kasulumu alisema tangu magari yazuiwe, hali ya uchumi imekuwa ngumu kwao kwa kuwa hakuna biashara inayouzika.

Mkuu wa Uhamiaji Wilaya ya Kyela, Vitalis Kumanya, alisema tayari hatua mbalimbali zimeanza kuchukuliwa na suala hilo litashughulikiwa kwa kuzingatia uhusiano baina ya nchi hizo.

Aliwaomba wananchi kuwa watulivu na kuepuka kuingia katika migogoro ambayo inaharibu uhusiano wa kidiplomasia na kibiashara.

Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Josephine Manase, alisema Serikali ya Malawi imeendelea kuzuia magari. Wanawasiliana ili kupata ufumbuzi wa mgogoro huo.

## HABARI KITAIFA



Mkurugenzi wa Taasisi ya Akili Platform Tanzania (APT) ya mkoani Tabora, Roghat Robert, akitoa elimu kwa wazazi wa watoto wenye ulemavu jinsi ya kulima kilimo cha mviringo kwa kuweka udongo kwenye viroba wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani mjini Nzega juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bunge laridhia mapendekezo TPA, DPW kuendeleza bandari

**Na Mwandishi Wetu**

BUNGE limeridhia mapendekezo ya Serikali ya Muungano Tanzania na Serikali ya Dubai, kushirikiana kiuchumi na kijamii kwa ajili ya uendelezaji na uboreshaji wa utendaji kazi katika Bandari ya Tanzania.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) iliingia Makubaliano ya awali (Memorandum of Understanding - MOU) na Kampuni ya DP World (DPW), inayomilikiwa na Serikali ya Dubai, Februari 28, 2022.

"Bunge katika mkutano wake wa 11 na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, linaazimia kuridhia makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Dubai kuhusu ushirikiano wa kiuchumi na kijamii kwa ajili ya uendelezaji na uboreshaji wa utendaji kazi katika Bandari Tanzania (The Intergovernmental Agreement Between the United Republic of Tanzania and the Emirate of Dubai Concerning Economic and Social," Azimio la Bunge linaeleza.

Makubaliano hayo yalikuwa na lengo la kubainisha maeneo mahsusi ya ushirikiano ili kuendeleza na kuboresha uendeshaji wa miundombinu ya kimkakati ya bandari za bahari na Maziwa Makuu, maeneo maalum ya kiuchumi (special economic zones), maeneo ya maegesho na utunzaji mizigo (logistics parks) na maeneo ya kanda za kibiashara.

Katika azimio hilo la Bunge, inaelezwa kuwa makubaliano hayo ya awali yalitokana na kudhihirika kwa tija na ufanisi uliopatikana kwenye bandari mbalimbali duniani, na Kampuni ya DPW imewekeza Dubai, Senegal, Msumbiji na nchi nyingine hali iliyosaidia huduma za uchukuzi kwa njia ya maji kuchangia kwa kiasi kikubwa kwenye pato la eneo au nchi husika.

Aidha, katika kuhakikisha Tanzania inapata tija stahiki kupitia huduma za bandari, Oktoba 25, 2022, Serikali ya Tanzania na Serikali ya Dubai zilisaini mkataba wa ushirikiano wa kiuchumi na kijamii kwa ajili ya uendelezaji na uboreshaji wa utendaji kazi wa bandari; mkataba unaolengwa kuridhiwa unabainisha vipengele muhimu ikiwa ni pamoja na: Mawanda ya ushirikiano na taasisi za utekelezaji; haki za kuendeleza, kusimamia na kuendesha shughuli za bandari; ridhaa za serikali; ushirikishaji wa wazawa, ajira na majukumu kwa jamii; kodi, tozo na ushuru nyinginezo.

Pia utatuzi wa migogoro; sheria zitakazosimamia mkataba; muda wa mkataba na usitishwaji wa mkataba; kuanza kutumika kwa mkataba; utekelezaji wa mkataba (IGA) ndani ya sheria za nchi na ubadilishanaji wa hati za uridhiaji.

Mkataba huo pia ni miongoni mwa jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita kwa lengo la kuendeleza na kuboresha utendaji na ufanisi wa bandari ili kuendana na dira ya serikali kuhusu kazi za bandari kuwa na mchango mkubwa katika mapato ya nchi na kuchagiza ukuaji wa sekta nyingine za kiuchumi nchini, sambamba na mabadiliko ya usimamizi na uendeshaji wa shughuli za kibandari.

"Serikali imeendelea kufanya jitihada mbalimbali ikiwamo uwekezaji mkubwa katika miundombinu ikijumuisha Mradi wa Maboresho ya Bandari Dar es Salaam, ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR na uboreshaji wa usafiri kwenye maziwa kwa lengo la kuchochea ukuaji wa uchumi na kuboresha ustawi wa Watanzania kwa ujumla," lilisema azimio hilo.

Bunge limesema maboresho katika sekta ndogo ya bandari yataiwezesha serikali kuendelea kutumia fursa ya kijiografia ya Tanzania kuzungukwa na bahari na maziwa ili kupata masoko na kuzihudumia nchi zisizo na bahari ikiwa ni pamoja na kuimarisha ushindani wa huduma za bandari na kuboresha shughuli za kijamii na kuichumi.

Manufaa ya mkutaba huo ni kuongeza fursa za ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja kutokana na uwekezaji mkubwa na ongezeko la shehena ya mizigo itakayopitia Bandari ya Dar es Salaam; kuongezeka kwa ufanisi katika uendelezaji na uboreshaji wa utendaji kazi na kuleta tija stahiki katika mnyororo wa thamani wa huduma za bandari nchini; kuongezeka kwa pato la Taifa kutokana na uboreshaji wa shughuli za kibandari.

Vile vile, kuongeza tija na kuwezesha mwendelezo wa miradi mikubwa ya kimkakati ambayo imekuwa ikijengwa na serikali kama Mradi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR), ujenzi wa meli za mizigo katika Maziwa Makuu na Mradi wa uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam; na kuchagiza na kuchochea ukuaji wa sekta nyingine za kiuchumi (Multiplier Effect) zikiwamo kilimo, utalii, viwanda, mifugo, uvuvi, biashara na usafirishaji na kuboresha ustawi wa Watanzania.

# ACT: Kikokotoo mafao ni kikwazo kwa wastaafu

**Na Julieth Mkireri,**
SHINYANGA

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema kanuni mpya za ukokotoaji mafao ni kitanzi kwa wastaafu.

Kimezitaja kanuni hizo ni kikwazo kwa kundi hilo na ndiyo sababu ya kuendelea kuwapo malalamiko ya wastaafu, wakidai kupunjwa mafao yao kutokana na kuanza kutekelezwa kwa kanuni hizo.

Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Tanzania Bara, Dorothy Semu, akizungumza katika mkutano uliofanyika mjini Shinyanga jana, alisema chama hicho kilieleza kwa kina namna kikokotoo kinavyokwenda kukwaza maisha ya wastaafu.

Alisema kutokana na uchambuzi uliofanywa na chama hicho, ni dhahiri kuwa kikotoo cha uwiano wa 1/580 kinaenda kupunguza mafao ya mwaka ya mtumishi aliyestaafu kwa asilimia 6.9.

"Kikokotoo hiki pia kwa uchambuzi wetu tumeona kitakwenda kupunguza malipo ya mkupuo ya kiinua mgongo kwa asilimia 50.5 kulinganisha na kanuni za awali.

"Vilevile, kinafupisha umri wa kuhudumiwa mstaafu kwa takribani miaka mitatu kutoka miaka 15.5 ya awali hadi 12.5," alieleza.

Kiongozi huyo pia alisema kuwa kupitia uchambuzi wao, kutakuwa na ongezeka katika posho ya kiinua mgongo ya kila mwezi kwa asilimia 24.7 lakini kwa kukokotolewa, jumla ya mafao atakayepokea kwa miaka 12.5 yanaongezeka kwa asilimia 0.6 pekee kutokana na kufupishwa kwa miaka mitatu tofauti na awali.

"ACT-Wazalendo tumeona ni lazima tuwasemee watumishi wa nchi hii. Wanafanya kazi kubwa, wanastahili jasho lao na si kifuta machozi. Ni lazima watu wajivunie kuwa watumishi na tunaamini kuwa mfumo wa hifadhi ya jamii husaidia kulinda maisha ya watu na kutoa uhakika wa kuishi vizuri.

"Hatupaswi kuwaadhibu wazee wetu kwa kukubali kanuni hizi kandamizi zinazokwenda kuwapunja mafao yao na kufupisha muda wa kuwahudumia kwa kuwakadiria kifo mapema zaidi," alisema.

Aliongeza kuwa chama hicho kinaitaka serikali kulipa madeni yote inayodaiwa na mifuko ya hifadhi ya jamii kwa mkupuo mmoja ili kuiwezesha mifuko kujiendesha na kuhudumia wateja wake kwa wakati.

"ACT-Wazalendo tunaitaka serikali kurejesha kanuni za zamani za mwaka 2017 na pia vyama vya wafanyakazi nchini vishikamane kama vilivyofanya miaka mitatu nyuma kupinga hili," alisisitiza.

Akizungumza katika mkutano huo, Kiongozi wa chama hicho, Zitto Kabwe, alisema wanaendelea kuitaka serikali iongeze fedha katika Mfuko wa Wakala wa Taifa wa Chakula (NFRA) ili ununue chakula cha kutosha kutoka kwa wakulima.

Zitto pia alisema maendeleo ya sekta ya madini yanatakiwa kwenda sambamba na maendeleo ya watu na maeneo yao kwa kuweka mikataba ya sheria na mgawanyo wa mirabaha.


GARI INAUZWA

Scania 114 hiub crene ton 6 boom 4

Yenye usajili Na: T 952 EBL




Contact: 0699 669990 or 0715 982272 Kinondoni Dar es Salaam.

MZEE PHABIAN HEVORD

# Babu, muuguzi mstaafu aliyegeuka gwiji mpekuataka Pugu Kinyamwezi

## ●Umaarufu wake; msomi pekee wa dampo




Phabian Hipority Hevord (83), akieleza jambo kwa mwandishi wa habari (hayupo pichani), kwenye dampo la Pugu Kinyamwezi jijini Dar es Salaam wiki iliyopita. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

**Na Christina Mwakangale**

**SEHEMU ya kwanza na ya pili yaripoti hii, ilikuwa na ufafanuzi wa watendaji na ushuhuda wa Nipashe kuhusu kinachoendelea katika dampo la Pugu Kinyamwezi. Endelea...**

WALIOKO katika dampo la Pugu Kinyamwezi, wengi wao ni wanaume wenye umri kuanzia miaka 35 na kuendelea. Kati ya watu 10 unaokutana nao katika dampo hilo, mmoja au wawili ni jinsi ya kike.

Katika udadisi wake ndani ya dampo hilo, Nipashe inakutana na mzee, amevaa mavazi meusi kuanzia nguo hadi buti. Bega lake la kulia limebeba mfuko mkubwa mweusi wa plastiki.

Anajitambulisha kwa uchangamfu, lakini maelezo yake kwa kiasi kikubwa yametekwa na lugha ya kigeni, kiingereza.

"Ninaitwa Phabian Hipority Hevord, nina umri wa miaka 83. Nimezunguka madampo mengi - Kunduchi, Mtoni, 'once upon a time' (hapo zamani za kale), nilijikuta ninakwenda madampo mengine, lakini ni miaka zaidi ya 35 nipo hapa (Pugu Kinyamwezi)," anasimulia.

Alipo sasa Phabian, hakutofautiani na alichowahi kufanyia kazi, yaani sekta ya afya, akiwa mtumishi katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) tangu enzi za uongozi wa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere. Alikuwa muuguzi.

"Dampo lilikuwa Kigogo, lipo 'near home' (karibu na nyumbani). Nikaona wenzangu wanapata mali, wanafanya kazi katika dampo. Mimi sichagui kazi, kusema sijui dokta.

"Nimesoma kwetu nilikozaliwa Matombo, Morogoro hadi darasa la nane mwaka 1958. Nikaja kusomea upadri huko Bagamoyo, kwa sababu ukoo wetu karibu wote wamesomea upadri.

"Nikaacha upadri. Nikasomea uuguzi mpaka mwaka 1960. Nimefanya kazi Ocean Road (Taasisi ya Saratani Ocean Road -ORCI) baadaye Muhimbili. Nimefanya kazi sehemu nyingi, Singida huko nilifanya kazi ya uuguzi," anasema Phabian.

Wenyeji wa eneo hilo, ambao wanafanya shughuli zao na mzee huyo, wanamtaja kwa sifa lukuki. Ndiye msomi pekee na ndiye mwenye umri mkubwa zaidi katika dampo hilo.

Phabian anasema anahitaji kustaafu na kama kungelikuwa na mafao kutokana na shughuli hiyo aliyoifanya kwa zaidi ya miaka 30, yangemfaa.

"Kama kungekuwa na kustaafu ningefurahi. Nina miaka 83 sio mchezo. Sasa hivi vijana wengi wako hapa katika dampo, ninasubiri waokote watoke, ndipo nami niingie niokote, sina nguvu ya kushindana nao.

"Kwa siku ninapata kama Sh. 500. Ikibidi nalala na njaa au mikate iliyotupwa ninaokota ninakula. Nina watoto sita, wote hawapo kwangu. Ni wakubwa sana. Mmoja mchungaji, wa kike wameolewa mikoani. Lakini mmoja akikupa fedha ni mara moja sana.

Phabian, mwenye makazi jirani na Shule ya Sekondari Pugu, kila siku hufunga safari kwa mguu kwenda katika dampo la Pugu Kinyamwezi, umbali wa takriban Km 20 kwenda na kurudi.

Anasema bidhaa ambazo huziokota ni mifuko ya plastiki ambayo baadaye huiuza kwa bei ya Sh. 300 kwa uzito wa kilo moja.

"Watu utakuta wanakucheka ila mimi ninajua ninachokifanya. Sasa nianze kuombaomba? Ninafanya hii kazi na nina amani tele!" Anasisitiza.

Kupata maradhi ya hapa na pale, ikiwamo magonjwa ya kuambukiza kama vile homa ya matumbo kwake ni nadra, anasema hakumbuki mara ya mwisho kuugua.

"Siumwi ovyo. Kuliko hata wale wanaofanya kazi sehemu za staha. Nina ufahamu na vyeti ninavyo ndani. Elimu yangu ya darasa la nane la zamani linamfikia nani na elimu yenu ya sasa vijana wa leo?

"Tumefundishwa na wazungu darasani. 'I'm not lying' (sidanganyi). Elimu yangu na uelewa unaweza kumfikia hata msomi wa chuo kikuu wa leo," anatamba.

Mmoja wa vijana wanaochambua taka katika dampo hilo, anaiona kazi hiyo kwake haifai. Ni fedheha, lakini kila kukicha anakwenda katika dampo hilo kusaka riziki.

"Jina langu usiliandike. Mimi ninafanya kazi hii. Ninapata fedha, ninapeleka nyumbani kuhudumia familia na wazazi wangu. Hakuna hata ndugu yangu mmoja anayejua ninafanya kazi hii na sitaki wajue.

"Sisi wanaume tunatafuta riziki hata mazingira magumu na hatarishi, mradi familia ipate mlo. Kazi hii ninaifanya kwa sababu ninapoamka asubuhi siwazi mtaji na sina mkataba na mtu unaonifunga. Mtaji ni afya yangu," anaeleza kijana huyo.

Anajitazama nguo zake kama amechafuka zaidi. Tayari mwonekano wake ni huo. Mikono yake pia ina tope la uchafu. Hana kifaa chochote cha kumkinga, kuanzia miguuni hadi kichwani. Harufu ya eneo hilo ni kali, ya uchafu.

### ATHARI KIAFYA

Daktari wa Binadamu kutoka Idara ya Afya ya Akili katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya (MZRH), Raymond Mgeni, anasema wanaojihusisha na shughuli za ina hiyo katika dampo wengi wao ni wagonjwa.

"Upo ugonjwa kama sikizofrenia ambao mhusika anakuwa anapenda kuokota vitu vichafu kutokana na dalili za ugonjwa wenyewe," anasema bingwa huyo. Msaikolojia Tiba, William Nkuhi, anasema kuna mambo mengi ya msingi ambayo watu wengi hawayajui kuhusu matatizo na magonjwa ya akili.

Anasema sio kila mtu anayeokota makopo au kufanya shughuli za kuchambua taka, ana magonjwa au matatizo ya akili.

"Mfumo wa maisha umechangia kwa kiasi kikubwa watu kufanya shughuli yoyote ile, hasa katika majiji makubwa kama Dar es Salaam. Kuna watu wanafanya kazi ambazo watu wengi hudhani kuwa wana matatizo au magonjwa ya akili.

Msaikolojia Tiba huyo anabainisha unyanyapaa miongoni mwa jamii umekuwa ukichochea watu hao kuitwa majina tofauti.

"Hawa watu huangukia katika shida za kisaikolojia kutokana na changamoto zingine za maisha na utumiaji wa dawa au vilevi.

"Wanaangukia katika ugonjwa sugu wa kisaikolojia unaitwa Substance and Drugs Abuse or Disorder. Ni kweli pia kuna watu hushinda katika majalala miaka na miaka na hawa tunawaweka katika kundi la watu wenye magonjwa ya akili, yanayosababishwa na mfumo wa maisha," anafafanua.

# Mbunge aipongeza serikali kuinua utalii

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MBUNGE wa Vwawa, Japhet Hasunga, ameipongeza serikali kwa kuimarisha sekta ya utalii na kuchangia kuongezeka idadi ya watalii kutoka milioni 1.5 mwaka 2021 hadi milioni 3.4 mwaka huu.

Amesema nchi kwa sasa inahitaji kuwa na mikakati ya kuwawezesha watalii kufurahia na kujionea vivutio vilivyopo bila bughudha yoyote ili kuchochea zaidi ukuaji wa sekta hiyo.

"Tunahitahji mikakati ya kuwawezesha watalii kula maisha. Tunahitaji kuimarika kwa utalii wa wanyamapori, milima, miamba kama kule Oldivai, mikutano, misitu, matibabu, vyuo, fukwe, wote huu ni utalii lakini maana ya utalii tunaupima kwa kuangalia waliotoka nje kuja ndani pamoja na kiasi cha fedha kilichoingia," alisema. Aliongeza kuwa ili sekta hiyo ilete manufaa zaidi, kufanywe maboresho katika utoaji wa huduma. Maeneo mengi, hasa hoteli bado hakuna huduma rafiki kwa watalii.

Alikumbusha umuhimu wa programu ya kuboresha utalii kusini kwa kutangaza zaidi vivutio na maliasili zinazopatikana huko.

"Kule Mbozi kuna kimondo kizuri, hapo Iringa tuna Ruaha. Tuna Mikumi, Rungwe, tuna milima, tuna kila ina ya vivutio. Lazima tuwekeze na huko nako zinapatikana fedha zinazoweza kuijenga nchi yetu.

Mbunge huyo aliyewahi kuwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii na baadaye Waziri wa Kilimo, alisema filamu ya Tanzania The Royal Tour imeleta faida kubwa nchini, akiitaka wizara husika kutumia mfano huo kutangaza vivutio zaidi.

Pia alipendekeza Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) ubadilishwe jina. Uwe mamlaka ya kusimamia misitu nchini.

# Waziri Masauni awasilisha maoni kwa Tume Hakijinai

**Na Restuta James**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni, amependekeza Jeshi la Polisi pamoja na vyombo vingine vinavyoshughulikia hakijinai visukwe ili wananchi wapate stahiki zao. Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana baada ya kuwasilisha maoni yake mbele ya Tume ya Hakijinai inayoongozwa na Jaji Mkuu mstaafu Mohamed Othman Chande, Waziri Masauni alisema pamoja na mambo mengine, amependekeza maboresho ya mfumo na mafunzo kwa vyombo hivyo, hususani Jeshi la Polisi.

Alisema: "Maoni yangu kwa ujumla ni mapendekezo ya kurekebisha mfumo, muundo na sheria katika vyombo hivyo ikiwamo utaratibu wa ajira, mafunzo, miundombonu stahiki, maslahi na mengineyo."

Taasisi za hakijinai zilizopo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni Jeshi la Polisi, Magereza na Uhamiaji. Waziri huyo alisema amewasilisha maoni mengi yanayolenga kutatua malalamiko ya wananchi dhidi ya vyombo hivyo.

"Yamelenga katika kuhakikisha tunakwenda kuleta mabadiliko kimfumo, kimuundo, kisheria, kiutaratibu na kikanuni kuwa na vyombo vya polisi na magereza ambavyo havina changamoto zinazotukabili hivi sasa," alisema.

Waziri Masauni alisema Jeshi la Polisi linakabiliwa na malalamiko ya kucheleweesha upelelezi wa kesi, utaratibu wa dhamana, jinsi ya kuhudumia mahabusu na ubambikaji wa kesi, ambayo yaliwasilishwa mbele ya Tume ya Jaji Chande. Anaaamini yatapatiwa ufumbuzi.

Alisema vyombo hivyo vinakabiliwa na changamoto za kiutendaji ikiwamo utaratibu wa ajira, maslahi ya askari, upandishaji vyeo, utaratibu wa mafunzo, vifaa vya kisasa na miundombinu.

Alisema mapendekezo yake yamegusa maeneo yote muhimu zikiwamo sheria, huku mengine yakiainisha maeneo mtambuka yanayogusa mamlaka nyingine za serikali.

Masauni ameitwa mbele ya Tume Chande, wakati ambao tayari imeanza kuchakata maoni kwa ajili ya kuandika ripoti ambayo itawasilishwa kwa Rais Samia Suluhu Hassan. Tume ya Jaji Chande ilianza kazi Februari Mosi mwaka huu na ilipaswa kumaliza kazi yake mwishoni mwa mwezi uliopita.



Baadhi ya wafanyabiashara wa mpakani mwa Tanzania na Malawi eneo la Kasumulu wilayani Kyela mkoani Mbeya jana waliandamana katika mpaka huo, wakishinikiza serikali ya Malawi kuyaachia magari 60 ya mizigo yaliyozuiwa ili kulipa tozo mpya za ukusanyaji mapato na usafirishaji mizigo zilizopitishwa na kuanza kutumika Aprili 18, mwaka huu. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Waziri ataka uwajibikaji kutatua migogoro hifadhini

**Na Jenifer Gilla,** DODOMA

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Mohamed Mchengerwa, amesema atawachukulia hatua viongozi wa taasisi za uhifadhi ikiwamo Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) watakaoshindwa kutatua changamoto za wanyama kuvamia makazi na kuharibu mali za wananchi katika hifadhi zao.

Aidha, amesema wizara hiyo inaandaa mkakati wa miaka 10 wa kushughulikia changamoto hizo pamoja na wa kuweka maofisa wanyama pori katika ngazi za vijiji na kata washughulikie kwa ukaribu migogoro hiyo ili wananchi wanaoishi katika maeneo ya uhifadhi waishi kwa amani. Mchengerwa aliyasema hayo juzi wakati akihitimisha mjadala wa makadirio ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka 2023/24 katika Kikao cha 40, Mkutano wa 11 wa Bunge la 12 jijini Dodoma.

Pia alisema atashughulikia viongozi ambao hawaendi kwenye maeneo yenye mgogoro ya wanyamapori kuzungumza na wananchi, ili kutafuta suluhisho licha ya wakazi wa maeneo hayo kupiga kelele za kuomba msaada kutoka kwao.

Alisema Jeshi la Uhifadhi limekuwa likichukua hatua za haraka kudhibiti wananchi kuingia ndani ya uhifadhi lakini wanyama wakali wanapovamia makazi ya watu na kuharibu rasilimali zao hatua za kuwadhibiti zinachelewa kuchukuliwa jambo ambalo si sahihi.

"Kama tunaweza kuchukua hatua za haraka dhidi ya wafugaji wanaoingiza ndani ya hifadhi vilevile tuchukue hatua za haraka kuwaondoa wanyama wakali katika maeneo ya wananchi," alisema.

Mchengerwa alisema wizara hiyo inaongozwa na Jeshi la Uhifadhi ambalo limepewa mafunzo ya kutosha na jukumu la kuhakikisha linadhibiti wanyamapori wanaovamia maeneo ya wananchi hivyo malalamiko ya wabunge kuhusu kadhia hiyo maana yake ni kuwa jeshi hilo halifanyi kazi yake ipasavyo.

Aliwahakikishia wabunge kuwa wizara inajipanga vizuri ili kumaliza changamoto zote zilizotajwa na wabunge kutoka kwenye majimbo yao, ili watakapokutana mwakani wazungumze namna watakavyoweza kukuza utalii wa nchi hiyo.

Katika kila wilaya nchini, alisema kuna maofisa wanyamapori, lakini anashangaa kusikia migogoro ya wanyama pori bado inaendelea kulalamikiwa na kuahidi wizara hiyo kurudisha misingi ya Baba wa Taifa, Julius Nyerere ya kuweka maofisa hao katika ngazi ya kata na vijiji ili waishughulikie kero hizo kwa ukaribu.

"Lakini ninachosisitiza hapa Spika nitamwomba Waziri Mkuu (Kassim Majaliwa) na wenzetu tuzungumze kama kuna uwezekano hawa maofisa wanyamapori warudishwe katika wizara hii (Maliasili na Utalii ), ili niweze kuwashughulikia vizuri katika maeneo yao, " alisema Mchengerwa.

Aidha, alisema wizara imeandaa mpango mkakati wa miaka 10 ambao umeainisha hatua za muda mfupi na muda mrefu za kushughulikia kero za uhifadhi, ili kuzimaliza kabisa na kuwatana maofisa uhifadhi kufanya kazi kwa weledi huku wakitanguliza ubinadamu mbele.

Alisema pia wameshaanza kufanya mapitio ya sheria na sera za uhifadhi, ili kufanya maboresho ya baadhi ya vifungu ikiwamo kuwabana askari wanaofanya vitendo vya uonevu kwa wananchi kinyume na Jeshi la Uhifadhi.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Mary Masanja, alisema wizara hiyo itafanya kazi kwa ukaribu na wananchi wanaoishi katika maeneo ya uhifadhi, ili kuhakikisha wanaimaliza kabisa migogoro yote inayohusiana na masuala ya uhifadhi.

Alisema wizara inajipanga kuainisha maeneo yanayoweza kuwa mahususi kwa ajili ya fukwe katika maeneo ya Mtwara, Lindi, Dar es Salaam, Pwani na Tanga na Kanda ya Ziwa ili zitumike ipasavyo katika utalii.

Pia alisema ili kukuza utalii wa kiberenge wizara imewekewa mshauri mwelekezi ambaye ameshaanza kufanya upembuzi na kupata mawazo ya wadau mbalimbali na kuangalia mazingira mazuri yatakayofaa kwa shughuli hiyo.

Naibu waziri huyo alisema wizara imeshaanza kujitanua katika utalii wa mali kale, katika maeneo ya Kilwa wameshaanzisha utalii wa meli pamoja na kuhamasisha wawekezaji ili kupanua wigo wa kuwahudumia watalii.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ushauri wa waziri kutangaza utamaduni wa asili una tija

**UTALII** una vivutio vingi na kama vitatangazwa vyote nchi inaweza kupata mapato mengi kupitia sekta hiyo.

Vivutio vya utalii vipo vya aina mbalimbali na hivyo ndivyo huwafanya watu wa mataifa mengine kupenda kutembelea Tanzania.

Hivi karibuni Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), Simai Mohammed Said, alitoa ushuari wa kuongeza nguvu kubwa katika kutangaza utamaduni wa asili, ikiwamo maajabu ya miti mbalimbali ili kuvutia watalii wengi zaidi kuja nchini.

Alitoa ushauri huo mwishoni mwa wiki, wakati akifungua maonyesho ya utalii ya kimataifa ya Karibu -Kill Fair 2023, yaliyofanyika kwa siku tatu jijini Arusha.

Kwa mujibu wa Simai, Tanzania imefungua fursa za utalii kutokana na fursa iliyotangazwa kupitia filamu ya The Royal Tour, ambayo imesaidia Zanzibar na Bara kwa pamoja kupata watalii wengi zaidi wanaotembelea vivutio vya utalii vikiwamo vya asili.

Alitaka nguvu iongezwe kuvitangaza vivutio hivyo kwa kuwa vitaongezea nchi watalii wengi zaidi ya sasa na Tanzania inavyo vingi ikiwamo miti yenye maajabu yake.

"Rais Samia Hassan Suluhu na Rais wa Zanzibar na Dk. Ali Hussein Mwinyi, wametangaza utalii na tunaamini msimu huu wa utalii utaleta ongezeko kubwa la utalii, hivyo naomba TRA (Mamlaka ya Mapato nchini) washirikiane na wadau wa utalii ili kuondoa matatizo wanayokumbana nayo wadau wa utalii nchini," alisisitiza waziri huyo.

Kwa mujibu wa waziri huyo, Zanzibar imechaguliwa kuwa eneo la utalii namba moja kwa Bara la Afrika katika msimu huu wa utalii na fursa hiyo itasaidia kunogesha utalii wa Tanzania Bara.

Katika kuweka msisitizo wa kauli ya Waziri, Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Richard Kayombo, anasema mamlaka hiyo itaendelea kushirikiana na wadau wa sekta ya utalii kama kaulimbiu isemavyo

"Utozaji kodi kwa njia ya kiungwana na kirafiki" na watazingatia maoni ya wadau hao wa utalii kwa kuboresha huduma za kodi.

Kadhalika katika kuzingatia hilo anasema utalii ukiporomoka sekta nyingine zitaporomoka, hivyo kila jambo linalohusiana na utalii, watahakikisha wanajenga mazingira rafiki kwa wafanyabiashara wa sekta hiyo.

Pia uwapo wa dawati la pamoja la utalii, TRA itazingatia hilo ili kuboresha huduma za utalii nchini na kuongeza mapato.

Kwa niaba ya waendesha utalii nchini, Mkurugenzi wa Kampuni ya Utalii ya Zara Tours, Zainab Ansell, anazungumzia haja kwa wadau wa sekta hiyo kuendelea kushirikiana na serikali kutangaza vivutio vilivyoko nchini ili watalii waendelee kumiminika.


Mkurugenzi Mwenza wa Kampuni ya Karibu Kili Fair, ambao walikuwa waandaaji wa maonyesho hayo, Dominic Shoo, anasema lengo la maonyesho hayo ni kutangaza vivutio vilivyoko nchini.

Maonyesho ya utalii yanashirikisha kampuni zaidi ya 370 kutoka nchi zaidi ya 12 duniani.

Hii ni hatua kubwa katika kukuza sekta ya utalii nchini ambayo husaidia nchi katika kuingiza pato la fedha za kigeni.

Hivyo, ni muhimu ushauri uliotolewa wa kutangaza vivutio vingi zaidi vya utalii uzingatiwe.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Bodaboda hawa ni kitisho cha maisha

**UJIO** wa pikipiki mijini na vijijini umeliondoa kundi kubwa la vijana lisilokuwa na ajira kwenye mahangaika kwa vile wengi wamechangamkia fursa ya kutoa huduma za usafiri kila mahali na kila wakati kwa kutumia pikipiki na bajaji.

Ni kwa njia hiyo vijana wengi ambao walikuwa na tatizo la kukosa ajira, walijitosa katika kazi ya kusafirisha abiria kwa kutumia pikipiki na bajaji ambazo ni maarufu zikifahamika kila mkoa na kijiji.

Kwa ujumla udereva wa bodaboda na bajaji umesaidia vijana hao kuwa na uhakika wa kuishi, kwani hupata fedha za kujikimu na kusaidia familia zao huku wakikuza uchumi wao na hata taifa pia.

Pamoja na fursa hiyo, zipo kasoro zinazokabili baadhi ya madereva hao wa ikiwamo tuhuma za wizi, kusababisha ajali zinazopoteza maisha yao na ya abiria au ulemavu wa kudumu lakini kusaidia kuonyesha watu wanaotafutwa ili wadhuriwe na hata kushiriki kwenye kubaka watoto.

Mtindo huo hasa wa wizi, umeendelea kuwapo katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam, ambapo huwapora mikoba wapita njia na kutokomea kusikojulikana.

Aidha, wanadaiwa kubeba mali za wizi, kushiriki kutorosha watoto kwa mfano wanafunzi na kuwapeleka kwenye mapagare wanaponajisiwa maeneo ya nje ya miji na hata vijijini pia ni mambo yanayowachafulia sifa.

Hivi karibuni katika barabara ya Mbezi Malamba Mawili kuelekea Segerea, jijini Dar Es Salaam, baadhi ya madereva wa bodaboda wanalalamikiwa kuwa wamekuwa wakiwapora wapita njia pesa, simu, mifuko wakati wa alfajiri na hata jioni giza linapoanza.

Uporaji huo au kukwapua mizigo ya watu, ni vitendo ambavyo vinaweza kuchangia ajira hiyo kuwa chungu kwao iwapo watabainika na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Wakumbuke Rais Samia Suluhu Hassan, aliwahi kuwaonya na kuwataka waendesha bodaboda hao kuacha kutumika katika ujambazi pamoja na kukwapua mizigo ya watu, ili kulinda heshima yao.

Rais Samia alishaweka wazi kuwa baadhi ya madereva bodaboda wamekuwa wakikwapua mizigo ya watu pamoja na vipochi hasa vya wanawake, hali ambayo inapoteza uaminifu mbele ya jamii.

Kauli hiyo ya mkuu wa nchi, ingetosha kuwafanya wabadilike, lakini cha ajabu ni kwamba, uporaji huo unaendelea kwenye baadhi ya maeneo likiwamo hilo ambalo nimelitaja.

Rais anawaita kama maofisa usafirishaji wa kitaifa, lakini inakuaje baadhi yao wawaharibie sifa kwa kutumika kukwapua na kupoteza mizigo ya watu au kutumika kwenye ujambazi?

Aliwataka wajilinde ili wasipoteze sifa njema, kwa kuwa wao watu muhimu katika taifa. Kwa wito huo, ni wazi Rais anakerwa na vitendo hivyo. Kwa maana hiyo ingekuwa ni vyema kama wangebadilika.

Ingefaa kila dereva wa bodaboda kutafakari na kuchukua hatua sahihi za kuachana na mtindo huo ambao kiukweli ni kwamba unaweza kutishia ajira yao hiyo ambayo inawawezesha kuendesha maisha.

Wapo baadhi ya madereva wanaodai kuwa wanaopora ni wale wanaoitwa 'deiwaka' ambao madereva halisi wakishachoka huwapa pikipiki, ili kujitafutia chochote, lakini badala yake wanapora watu.

Iwapo hilo lina ukweli ndani yake, walioajiriwa kuendesha boda boda wasikubali kuharibiwa sifa njema, kwa sababu ya huruma ya kutaka kuwasaidia marafiki zao wanaozitumia kupora watu.

Wakumbuke kuwa udereva wa bodaboda kwa sasa ni ajira, hivyo ni vyema kama madereva wataiheshimu, kwa kuepuka kujiingiza katika vitendo vya uporaji na kuhatarisha maisha yao.

## Mgodi watoa elimu kwa wananchi taka za plastiki

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Geita Gold Mining Limited (GGML), moja ya migodi maarufu ya AngloGold Ashanti nchini, imeadhimisha Siku ya Mazingira Duniani kwa kutoa elimu kuhusu aina mbalimbali za taka za plastiki na ugawaji wa vifaa vya kuhifadhi taka kwa lengo la kuwawezesha wananchi kutenganisha ipasavyo taka za plastiki.

Siku ya Mazingira Duniani ambayo huadhimishwa kila mwaka tarehe 5 Juni, ni tukio muhimu la kimataifa lililoandaliwa na Mpango wa Mazingira wa Umoja wa Mataifa, mwaka huu kaulimbiu ikiwa "tokomeza uchafuzi wa mazingira unaotokana na taka za plastiki".

Ni kaulimbiu inayolenga kusisitiza taka za plastiki ni tatizo la kimataifa ambalo linatishia mazingira, wanyamapori na afya ya binadamu.

Akizungumza katika maadhimisho hayo yaliyofanyika mjini Geita kwa kuwashirikisha wafanyakazi wa GGML na mamlaka za mitaa, Meneja Mazingira wa Mgodi huo, Yusuph Mhando, alisema GGML inafahamu uchimbaji madini una athari ya moja kwa moja kwa mazingira kwa kuwa rasilimali za ardhi na maji zinahitaji kuendelezwa.

Alisema kampuni hiyo imejizatiti katika utunzaji wa mazingira na imechukua hatua mbalimbali ili kupunguza mwelekeo wake wa mazingira na kuongeza mchango wake chanya kwa jamii zinazoizunguka.

"Moja ya hatua hizo ni usimamizi wa taka za plastiki kutoka vyanzo mbalimbali kama vile vifungashio, vifaa vya kujikinga, chupa za maji na vyombo vya chakula. Kampuni pia inatoa mafunzo kwa wafanyakazi na makandarasi wote kutenganisha na kutupa aina tofauti za taka kwa kutumia mapipa yenye alama za rangi na lebo. Wafanyakazi wote na makandarasi hupokea mafunzo ya mazingira ili kuhakikisha uzingatiaji wa sera na taratibu za usimamizi wa taka.

Alisema GGML inafanya kazi kwa pamoja ili kuongeza uelewa kuhusu umuhimu wa kupunguza, kutumia tena na kuchakata plastiki.

"Tunajivunia kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani na kushirikisha jamii zinazozunguka mgodi katika kuendeleza desturi nyetu ya kulinda na kuhifadhi mazingira yetu. Tunaamini kwa kuwaelimisha na kuwawezesha wananchi kutenganisha ipasavyo taka za plastiki tunaweza kuleta mabadiliko chanya katika vita dhidi ya uchafuzi wa plastiki.

"Pia tunahimiza kila mtu kuzingatia kanuni ya 3Rs: Punguza, Tumia Tena na Usafishaji plastiki kila inapowezekana," alisema.

Kiongozi huyo alisema GGML inachukua jukumu lake la kupunguza athari zake za mazingira kwa umakini na imejitolea kuwajibika kwa usimamizi wa mazingira.

Aliongeza kuwa mgodi huo umekuwa ukifanya kazi nchini kwa zaidi ya miaka 20 na ni miongoni mwa walipakodi wakubwa na wanaokidhi viwango vinavyozingatia sheria nchini.

GGML inaajiri zaidi ya watu 5,000 moja kwa moja na kupitia makandarasi na takriban asilimia 98 kati yao ni raia wa Tanzania.

# Mitaala UDOM kufumuliwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof.Adolf Mkenda, amezindua kamati za kusaidia Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) kufanya maboresho ya mitaala ili kuzalisha wasomi wanaokidhi soko la ajira ndani na nje ya nchi.

Katika uzinduzi huo jana, Prof. Mkenda alisema maboresho hayo yanafanywa kupitia Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET).

Alisema Tanzania ya sasa inahitaji wasomi wenye uelewa. Siyo wasomi wanaomaliza bila ujuzi. Prof. Mkenda alisema tayari wizara imeshakamilisha mitaala ya kuanzia elimu ya awali hadi kidato cha sita na vyuo vya ualimu na sasa wanapitia masahihisho.

"Vyuo vya kati vimekamilisha mitaala hasa katika mageuzi kulingana na mtazamo wa elimu ambayo inatarajia kupata watu wenye ujuzi na uelewa,"alisema.

Awali, Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Lughano Kusiluka, alisema mradi wa HEET unafadhiliwa na Benki ya Dunia kwa ajili ya kupitia mitaala ya vyuo ili kufanyia maboresho kwa ajili ya kupata 'wahitimu wa viwango'.

"Lengo letu ni kufanya mageuzi makubwa yatakayopelekea uzalishaji wa wasomi wenye kukidhi soko la Tanzania na nje ya nchi ambao hatutokuwa na hofu nao.

"Tunataka kuwa na wahitimu walioiva, tumekuwa tukishinda kwa wahitimu wetu katika maeneo mengi lakini dunia inazunguka, lazima tujipange katika mitaala yetu. Ninasema UDOM ipo tayari kwa mageuzi hayo," alisema.

Prof. Kusiluka alisema wataalamu waliopewa nafasi katika kamati hizo wanapaswa kujituma na kuangalia mahitaji ya dunia wanapotengeneza mitaala hiyo.

Mratibu wa HEET chuoni hapo, Prof. Razack Lokina, alisema mitaala watakayokuja nayo itakuwa ya kisasa, yenye kuifanya elimu ya mhitimu kuwa bora katika soko la ajira.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Jenipha Omolo na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Alphayo Kidata, wakiteta jambo wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya matumizi ya mifumo ya kielektroniki ya usimamizi wa kodi ya zuio iliyoboreshwa kwa wahasibu kutoka wizara, idara, wakala na taasisi za serikali yaliyoandaliwa na TRA kwa kushirikiana na wizara hiyo mkoani Dodoma. **PICHA: TRA**

# TRA, MRA wazindua mfumo wa kubadilishana taarifa

**Na Mwandishi Wetu,** KYELA

NAIBU Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mcha Hassan Mcha na Mkurugenzi Mtendaji wa Huduma za Shirika wa Mamlaka ya Mapato Malawi (MRA), Agnes Phiri, wamezindua mfumo wa kubadilishana taarifa kwa njia ya kielektroniki.

Hafla ya uzinduzi huo ilifanyika juzi katika Kituo cha Forodha cha Pamoja (OSBP) Kasumulu kilichoko Kyela mkoani Mbeya.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Naibu Kamishna Mkuu wa TRA, Mcha alisema mfumo huo utasaidia kuokoa muda na gharama, pia kuongeza ufanisi wa biashara ya mipakani na kuchochea ukuaji wa uchumi wa kikanda.

Mkurugenzi Mtendaji Huduma za Shirika wa MRA, Agnes, alisema mfumo huo unalenga kurahisisha michakato ya forodha, kukuza uwazi na kuwezesha shughuli za biashara.

"Pia unalenga kuunganishwa kwa TRA-TANCIS na MRA ASYCUDA World kutaleta mapinduzi katika mchakato wa kibali, kunufaisha wafanyabiashara na watu binafsi Tanzania na Malawi," alisema.

Mradi huo umefadhiliwa na Uingereza kupitia Trademark Africa. Mwakilishi wa wafadhili hao ambaye ni Mkurugenzi wa Trademark Africa nchini, Dk. Jovin Mwemezi alipongeza umuhimu na manufaa ya mradi huo akisema "...ninafuraha kuunga mkono mradi huu wa msingi utakaoleta mapinduzi ya biashara ya mipakani kati ya Malawi na Tanzania.

Wasafirishaji wa mizigo wamepongeza jitihada hizo kwa kuwa kubadilishana taarifa kwa njia ya kielektroniki ni muhimu kwa tasnia ya usafirishaji wa mizigo baina ya nchi na nchi.

Wamesena unawezesha kutoa huduma za haraka, zenye ufanisi zaidi kwa wateja, kuongeza ushindani wa biashara na kukuza biashara ya kimataifa.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
ISO 9001:2015 Certified

## *KUMB: PPR/2023 - 6/1*

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI KUANZIA JUMATANO, TAREHE 7 JUNI 2023

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia Jumatano, **tarehe 7 Juni 2023 saa 6:01 usiku.** Pamoja na kutambua bei hizo, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

(a) Kwa Juni 2023, bei za rejareja za mafuta ya dizeli na mafuta ya taa yaliyopokelewa kupitia **Bandari ya Dar es Salaam** zimeshuka kwa shilingi 209/Lita na shilingi 1/lita, mtawalia, ikilinganishwa na bei za toleo la tarehe 3 Mei 2023. Bei ya petroli imeongezeka kwa shilingi 2/lita ikilinganishwa na bei ya toleo la tarehe 3 Mei 2023.

(b) **Kwa Mikoa ya Kaskazini (Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara),** bei ya rejareja ya mafuta ya dizeli kwa Juni 2023 imeshuka kwa shilingi 198/Lita wakati bei ya mafuta ya petroli katika mwezi husika imeongezeka kwa shilingi 156/lita ikilinganishwa na bei za toleo la tarehe 3 Mei 2023. Kwa mafuta ya taa, waendeshaji wa vituo katika mikoa ya Kaskazini wanashauriwa kuchukua mafuta hayo kutokea bandari ya Dar es Salaam. Hivyo, bei za rejareja za mafuta ya taa katika mikoa hiyo zimezingatia gharama za kupokelea mafuta hayo kupitia Bandari ya Dar es Salaam na gharama za usafirishaji mpaka mikoa husika.

(c) **Kwa Mikoa ya Kusini (Mtwara, Lindi, na Ruvuma),** hakuna shehena ya bidhaa za mafuta iliyopokelewa kupitia bandari ya Mtwara kwa Mei 2023. Hivyo, bei ya rejareja ya dizeli kwa Juni 2023 itaendelea kuwa ni ile iliyotangazwa katika toleo la tarehe 3 Mei 2023. Kutokana na upungufu wa bidhaa ya petroli katika maghala ya kuhifadhi mafuta yaliyopo Mtwara, waendeshaji wa vituo vya mafuta katika mikoa ya kusini wanashauriwa kuchukua mafuta hayo kutoka katika bandari ya Dar es Salaam. Hivyo, bei za rejareja za mafuta ya petroli katika mikoa hiyo zimezingatia gharama za petroli iliyopokelewa kupitia Bandari ya Dar es Salaam na gharama za usafirishaji mpaka mikoa husika. Aidha, kwa kuwa hakuna matanki ya kuhifadhia mafuta ya taa katika bandari ya Mtwara, waendeshaji wa vituo vya mafuta katika mikoa ya kusini wanashauriwa kuchukua mafuta hayo kutoka katika bandari ya Dar es Salaam na hivyo bei za rejareja za mafuta ya taa katika mikoa hiyo itakuwa kulingana na gharama za kupokelea mafuta hayo kupitia Bandari ya Dar es Salaam na gharama za usafirishaji mpaka mikoa husika.

Bei za miji, wilaya na mikoa ni kama zinavyooneshwa katika Jedwali Na. 1. Tofauti ya bei kutoka sehemu moja kwenda nyingine inatokana na tofauti ya bei ya mafuta katika bandari ambayo mafuta yamepakiwa na gharama za usafirishaji.
Mabadiliko haya ya bei yanachangiwa na kubadilika kwa bei za mafuta katika soko la dunia, gharama za uagizaji (BPS Premium) na thamani ya Shilingi dhidi ya Dola ya Marekani.
Katika kutekeleza bei hizi, wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta kwa jumla na rejareja pamoja na jamii kwa ujumla wanatakiwa kuzingatia yafuatayo: -

i. EWURA inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli kwa eneo husika zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba ***152*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.

ii. Kwa mujibu wa **Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015,** kifungu namba 166, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.

iii. Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu **bei hizo zisivuke bei kikomo (Price cap) au kushuka chini ya bei iliyoruhusiwa (Floor Price) kama ilivyokokotolewa kwa mujibu wa Kanuni za EWURA za Kupanga Bei za Mafuta za Mwaka 2022 zilizotangazwa kupitia Gazeti la Serikali Na. 57 la tarehe 28 Januari 2022.**

iv. Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**

v. Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (Electronic Fiscal Pump Printers) na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mauzo ya mafuta ya petroli.

vi. Wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta kwa rejareja **wanatakiwa kuuza mafuta kwa bei inayooneshwa katika Jedwali Na. 1. Hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mfanyabiashara yoyote atakayekiuka AGIZO hili.**

vii. Wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta kwa jumla **wanatakiwa kuuza mafuta kwa bei inayooneshwa katika Jedwali Na. 2 isipokuwa kwa wateja wenye msamaha wa kodi. Hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mfanyabiashara yoyote atakayekiuka AGIZO hili.**

### JEDWALI 1: BEI KIKOMO ZA REJAREJA KWA SHILINGI/LITA

| Mji | Bei Kikomo | | |
|---|---|---|---|
| | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa |
| **Dar es Salaam** | **2,873** | **2,662** | **2,829** |
| **Arusha** | **2,969** | **2,759** | **2,913** |
| Arumeru (Usa River) | 2,969 | 2,759 | 2,913 |
| Karatu | 2,987 | 2,777 | 2,931 |
| Longido | 2,980 | 2,770 | 2,924 |
| Monduli | 2,974 | 2,764 | 2,918 |
| Monduli-Makuyuni | 2,979 | 2,769 | 2,923 |
| Ngorongoro (Loliondo) | 3,054 | 2,843 | 3,005 |
| **Coast (Kibaha)** | **2,878** | **2,667** | **2,833** |
| Bagamoyo | 2,884 | 2,673 | 2,840 |
| Bagamoyo (Miono) | 2,915 | 2,704 | 2,871 |
| Bagamoyo (Mbwewe) | 2,896 | 2,685 | 2,852 |
| Chalinze Junction | 2,887 | 2,677 | 2,843 |
| Chalinze Township (Msata) | 2,892 | 2,681 | 2,847 |
| Kibiti | 2,894 | 2,683 | 2,849 |
| Kisarawe | 2,880 | 2,669 | 2,836 |
| Mkuranga | 2,883 | 2,672 | 2,839 |
| Rufiji | 2,901 | 2,690 | 2,857 |
| **Dodoma** | **2,932** | **2,721** | **2,888** |
| Bahi | 2,939 | 2,728 | 2,895 |
| Chamwino | 2,927 | 2,716 | 2,883 |
| Chemba | 2,959 | 2,748 | 2,914 |
| Kondoa | 2,965 | 2,754 | 2,921 |
| Kongwa | 2,929 | 2,718 | 2,885 |
| Mpwapwa | 2,933 | 2,722 | 2,889 |
| Mpwapwa (Chipogoro) | 2,945 | 2,734 | 2,901 |
| Mtera (Makatopora) | 2,951 | 2,740 | 2,907 |
| Mvumi | 2,939 | 2,728 | 2,894 |
| **Geita** | **3,039** | **2,828** | **2,994** |
| Bukombe | 3,028 | 2,817 | 2,983 |
| Chato | 3,060 | 2,849 | 3,015 |
| Mbogwe | 3,077 | 2,866 | 3,032 |
| Nyang'hwale | 3,054 | 2,843 | 3,009 |
| **Iringa** | **2,937** | **2,726** | **2,893** |
| Ismani | 2,943 | 2,732 | 2,898 |
| Kilolo | 2,942 | 2,731 | 2,897 |
| Mufindi (Mafinga) | 2,947 | 2,737 | 2,903 |

## TANGAZO


| Mji | Bei Kikomo | | |
|---|---|---|---|
| | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa |
| Mufindi (Igowole) | 2,956 | 2,745 | 2,912 |
| **Kagera (Bukoba)** | **3,089** | **2,878** | **3,044** |
| Biharamulo | 3,063 | 2,852 | 3,019 |
| Karagwe (Kayanga) | 3,105 | 2,894 | 3,061 |
| Kyerwa (Ruberwa) | 3,111 | 2,900 | 3,067 |
| Muleba | 3,089 | 2,878 | 3,044 |
| Ngara | 3,077 | 2,866 | 3,032 |
| Misenyi | 3,097 | 2,886 | 3,053 |
| **Katavi (Mpanda)** | **3,031** | **2,820** | **2,987** |
| Mlele (Inyonga) | 3,013 | 2,802 | 2,968 |
| Mpimbwe (Majimoto) | 3,050 | 2,839 | 3,006 |
| Tanganyika (Ikola) | 3,049 | 2,838 | 3,005 |
| **Kigoma** | **3,036** | **2,825** | **2,991** |
| Uvinza (Lugufu) | 3,026 | 2,815 | 2,982 |
| Muyobozi Village (Uvinza) | 3,034 | 2,823 | 2,990 |
| Ilagala Village (Uvinza) | 3,036 | 2,826 | 2,992 |
| Buhigwe | 3,034 | 2,823 | 2,990 |
| Kakonko | 3,036 | 2,826 | 2,992 |
| Kasulu | 3,045 | 2,834 | 3,000 |
| Kibondo | 3,042 | 2,831 | 2,998 |
| **Kilimanjaro (Moshi)** | **2,959** | **2,748** | **2,903** |
| Hai (Bomang'ombe) | 2,962 | 2,752 | 2,906 |
| Mwanga | 2,952 | 2,741 | 2,896 |
| Rombo (Mkuu) | 2,975 | 2,765 | 2,924 |
| Same | 2,945 | 2,735 | 2,889 |
| Siha (Sanya Juu) | 2,965 | 2,755 | 2,909 |
| **Lindi** | **2,932** | **3,013** | **2,888** |
| Lindi-Mtama | 2,950 | 3,018 | 2,906 |
| Kilwa Masoko | 2,907 | 3,037 | 2,863 |
| Liwale | 2,953 | 3,049 | 2,909 |
| Nachingwea | 2,961 | 3,033 | 2,917 |
| Ruangwa | 2,963 | 3,040 | 2,919 |
| **Manyara (Babati)** | **3,003** | **2,793** | **2,951** |
| Hanang (Katesh) | 3,014 | 2,803 | 2,962 |
| Kiteto (Kibaya) | 3,018 | 2,808 | 2,962 |
| Mbulu | 3,016 | 2,806 | 2,964 |
| Simanjiro (Orkasumet) | 3,035 | 2,825 | 2,983 |
| **Mara (Musoma)** | **3,039** | **2,828** | **2,995** |
| Musoma Vijijini (Busekela) | 3,052 | 2,841 | 3,007 |
| Rorya (Ingirijuu) | 3,046 | 2,835 | 3,002 |
| Rorya (Shirati) | 3,054 | 2,843 | 3,010 |
| Bunda | 3,030 | 2,820 | 2,986 |
| Bunda (Kisorya) | 3,043 | 2,832 | 2,998 |
| Butiama | 3,036 | 2,825 | 2,992 |
| Serengeti (Mugumu) | 3,047 | 2,837 | 3,003 |
| Tarime | 3,048 | 2,837 | 3,003 |
| Tarime (Kewanja/Nyamongo) | 3,053 | 2,842 | 3,009 |
| **Mbeya** | **2,980** | **2,769** | **2,936** |
| Chunya | 2,990 | 2,779 | 2,946 |
| Chunya (Makongolosi) | 2,995 | 2,784 | 2,951 |
| Chunya (Lupa Tingatinga) | 2,997 | 2,786 | 2,953 |
| Kyela | 2,996 | 2,785 | 2,952 |
| Mbarali (Rujewa) | 2,965 | 2,754 | 2,920 |
| Rujewa (Madibira) | 2,978 | 2,767 | 2,933 |
| Rujewa (Kapunga) | 2,974 | 2,763 | 2,930 |
| Rungwe (Tukuyu) | 2,989 | 2,778 | 2,945 |
| Busokelo (Iwangwa) | 2,993 | 2,782 | 2,948 |
| **Morogoro** | **2,898** | **2,687** | **2,854** |
| Mikumi | 2,914 | 2,703 | 2,870 |
| Kilombero (Ifakara) | 2,936 | 2,725 | 2,892 |
| Kilombero (Mlimba) | 2,959 | 2,748 | 2,914 |
| Kilombero (Mngeta) | 2,948 | 2,737 | 2,903 |
| Ulanga (Mahenge) | 2,947 | 2,736 | 2,902 |
| Malinyi | 2,957 | 2,746 | 2,913 |
| Kilosa | 2,917 | 2,706 | 2,872 |
| Gairo | 2,917 | 2,706 | 2,872 |
| Mvomero (Wami Sokoine) | 2,909 | 2,698 | 2,864 |
| Mvomero (Sanga Sanga) | 2,898 | 2,687 | 2,854 |
| Turian | 2,923 | 2,712 | 2,879 |
| **Mtwara** | **2,946** | **3,000** | **2,901** |
| Nanyumbu (Mangaka) | 2,995 | 3,036 | 2,950 |
| Masasi | 2,971 | 3,016 | 2,927 |
| Newala | 2,978 | 3,021 | 2,933 |
| Tandahimba | 2,971 | 3,014 | 2,927 |
| Nanyamba | 2,971 | 3,014 | 2,927 |
| **Mwanza** | **3,023** | **2,813** | **2,979** |
| Kwimba | 3,041 | 2,830 | 2,997 |
| Magu | 3,032 | 2,821 | 2,987 |
| Misungwi | 3,018 | 2,807 | 2,973 |
| Misungwi (Mbarika) | 3,028 | 2,817 | 2,984 |
| Sengerema | 3,056 | 2,845 | 3,012 |
| Ukerewe | 3,083 | 2,872 | 3,039 |
| **Njombe** | **2,966** | **2,755** | **2,921** |
| Njombe (Kidegembye) | 2,986 | 2,775 | 2,942 |
| Ludewa | 3,004 | 2,793 | 2,959 |
| Makambako | 2,958 | 2,747 | 2,914 |
| Makete | 2,997 | 2,786 | 2,952 |
| Wanging'ombe (Igwachanya) | 2,964 | 2,753 | 2,919 |
| **Rukwa (Sumbawanga)** | **3,046** | **2,835** | **3,002** |
| Sumbawanga Rural (Mtowisa) | 3,046 | 2,835 | 3,002 |
| Kalambo (Matai) | 3,053 | 2,843 | 3,009 |
| Nkasi (Namanyele) | 3,060 | 2,849 | 3,015 |
| Nkasi (Kirando) | 3,069 | 2,858 | 3,025 |
| **Ruvuma (Songea)** | **2,997** | **3,085** | **2,952** |
| Mbinga | 3,009 | 3,098 | 2,965 |
| Namtumbo | 3,002 | 3,076 | 2,958 |
| Nyasa (Mbamba Bay) | 3,020 | 3,123 | 2,975 |
| Tunduru | 2,976 | 3,050 | 2,932 |
| **Shinyanga** | **3,002** | **2,791** | **2,958** |
| Kahama | 3,007 | 2,796 | 2,962 |
| Kishapu | 3,010 | 2,799 | 2,966 |
| Ushetu (Nyamilangano) | 3,019 | 2,808 | 2,974 |
| Ushetu (Kangeme Village) | 3,024 | 2,813 | 2,980 |
| Salawe | 3,016 | 2,805 | 2,972 |
| **Simiyu (Bariadi)** | **3,020** | **2,809** | **2,976** |
| Busega (Nyashimo) | 3,032 | 2,821 | 2,988 |
| Itilima (Lagangabilili) | 3,020 | 2,809 | 2,976 |
| Maswa | 3,014 | 2,803 | 2,970 |
| Meatu (Mwanhuzi) | 3,025 | 2,814 | 2,981 |
| **Singida** | **2,964** | **2,753** | **2,920** |
| Iramba | 2,976 | 2,765 | 2,932 |
| Manyoni | 2,949 | 2,738 | 2,904 |
| Itigi (Mitundu) | 2,964 | 2,753 | 2,920 |
| Ikungi | 2,959 | 2,749 | 2,915 |
| Mkalama (Nduguti) | 2,989 | 2,778 | 2,944 |
| **Songwe (Vwawa)** | **2,990** | **2,779** | **2,945** |
| Songwe (Mkwajuni) | 2,997 | 2,786 | 2,952 |
| Ileje | 2,994 | 2,783 | 2,949 |
| Momba (Chitete) | 2,999 | 2,788 | 2,954 |
| Tunduma | 2,994 | 2,783 | 2,949 |
| **Tabora** | **2,982** | **2,771** | **2,937** |
| Igunga | 2,981 | 2,770 | 2,937 |
| Kaliua | 2,995 | 2,784 | 2,950 |
| Ulyankulu | 2,992 | 2,781 | 2,948 |
| Nzega | 2,992 | 2,781 | 2,948 |
| Sikonge | 2,990 | 2,779 | 2,946 |
| Urambo | 2,991 | 2,781 | 2,947 |
| Uyui | 2,988 | 2,777 | 2,943 |
| Mpyagula | 3,013 | 2,802 | 2,969 |
| **Tanga** | **2,919** | **2,708** | **2,875** |
| Handeni | 2,933 | 2,723 | 2,854 |
| Kilindi | 2,948 | 2,738 | 2,889 |
| Korogwe | 2,924 | 2,714 | 2,868 |
| Lushoto | 2,934 | 2,724 | 2,878 |
| Mkinga (Maramba) | 2,934 | 2,723 | 2,889 |
| Muheza | 2,919 | 2,708 | 2,875 |
| Pangani | 2,926 | 2,715 | 2,882 |

**JEDWALI 2: BEI KIKOMO ZA JUMLA KWA SHILINGI/LITA**

| Bandari | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa |
|---|---|---|---|
| Dar es Salaam | 2,742.31 | 2,531.65 | 2,698.35 |
| Tanga | 2,781.28 | 2,571.26 | - |
| Mtwara | 2,662.38 | 2,867.94 | - |

Dkt. James A. Mwainyekule

**MKURUGENZI MKUU- EWURA**



# Wamjengea nyumba mwalimu aliyekuwa akilala ofisini

**Na Shaban Njia,** KISHAPU

WANAKIJIJI wa Miyuguyu Kata ya Kiloleli wilayani Kishapu mkoani Shinyanga wamejenga nyumba maalumu kwa ajili ya mwalimu aliyekuwa akiishi katika moja ya ofisi za Shule ya Msingi Miyuguyu.

Lengo la ujenzi wa nyumba hiyo ni kumnusuru na adha ya kuendelea kuishi ofisini hapo na kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Shule hiyo ina wanafunzi 524, madarasa sita, walimu sita, kati ya hao mwalimu wa kike ni mmoja na nyumba za walimu tatu, kati ya hizo mbili zilijengwa na serikali na moja imejengwa na wananchi, huku ikiwa na uhaba wa walimu 11 wa masomo ya sayansi na hisabati.

Akizungumza juzi katika kikao cha tathmini ya hali ya utendaji kazi wa Kituo cha Taarifa na Maarifa cha kijiji hicho, ambapo baadhi ya wajumbe walisema mojawapo ya mafanikio waliyoyapata ni kujenga nyumba hiyo aliyekuwa akiishi katika moja ya ofisi za shule hiyo.

Mmoja wa wajumbe hao, Agnes Kwilasa alisema ujenzi wa nyumba hiyo unatokana na uwapo wa hamasa ya Bunge la Jamii ambalo limeundwa kupitia Kituo cha Taarifa na Maarifa kwa kushirikiana na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) hali iliyofanya wananchi kuhamasika, kuchangia na kujenga nyumba hiyo.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Miyuguyu, Hamis Mashauri, alisema tatizo la uhaba wa nyumba za walimu katika Shule ya Msingi Miyuguyu linasababisha walimu kushindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo, ndiyo sababu ya wanakijiji kuhamasika na kujenga nyumba hiyo ili kuboresha mazingira bora ya kufanyia kazi kwa walimu wao.

Mwalimu aliyejengewa nyumba hiyo, Getrude Missana alisema awali alikuwa akiishi katika moja ya ofisi katika shule hiyo hali iliyokuwa inamuwia vigumu kutekeleza majukumu yake na kusababisha kuamka alfajiri kwa kukwepa wanafunzi kumuona akitoka ndani.

Ofisa kutoka TGNP, Degratius Temba akizungumza na wajumbe wa Kituo cha Taarifa na Maarifa alipongeza jitihada zilizofanikisha kujengwa kwa nyumba ya mwalimu ambaye awali alikuwa akiishi shuleni na kuwasihi kuendelea kushirikiana na serikali katika kutatua matatizo yanayoikabili sekta ya elimu hasa shuleni.



Wafanyakazi wa mgodi wa dhahabu wa Sotta na wakazi wa Kijiji cha Ngoma wilayani Sengerema mkoani Mwanza, wakiokota taka za plastiki kwa lengo la kusafisha mazingira kijijini hapo juzi, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## DC ahimiza ubora ukarabati Uwanja wa Ndege Shinyanga

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Wilaya ya Shinyanga, Johari Samizi, amewaagiza viongozi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kuhakikisha wanaukarabati Uwanja wa Ndege wa Shinyanga katika viwango vyenye ubora wa kuendana na thamani ya fedha.

Alibainisha hayo juzi wakati wa kikao cha wadau wa anga kilicholenga kujadili juu ya ukarabati wa Uwanja wa Ndege wa Ibadakuli Manispaa ya Shinyanga, ambao tayari umetengewa zaidi ya Sh. milioni 49.

Alisema kuwa serikali imetafuta fedha kutoka kwa wafadhili kwa lengo la kukamilisha ujenzi wa uwanja huo wa ndege wa Ibadakuli, ambao ni shauku kwa wananchi wa Mkoa wa Shinyanga na wafanyabiashara kupata usafiri wa anga kuwa karibu na kuagiza uwanja huo ujengwe kwa kiwango bora.

"Tunamshukuru sana Rais Samia Suluhu kwa kutuletea fedha kwa ajili ya ujenzi wa uwanja wa ndege ni muda mrefu sasa wananchi wa Shinyanga wamekuwa na shauku kubwa ya kupata uwanja wa ndege kwani wamekuwa wakilazimika kusafiri kwenda mkoani Mwanza kupanda ndege umbali wa kilomita 164," alisema Johari.

Meneja Mradi wa Viwanja vya Ndege kutoka Wakala wa Barabara Tanzania (TANROAD) makao makuu, Mhandisi Neema Joseph, alisema ujenzi wa uwanja huo utafanyiwa maboresho makubwa ukiwa na pamoja na upanuzi wa uwanja, pamoja na ujenzi wa jengo la kusubiri abiria na miundombinu ya barabara kwa kiwango cha lami.

Alisema ujenzi wa uwanja huo utachukua muda wa miezi 18 hadi kukamilika kwake, ambao utakwenda hadi Oktoba 3, 2024 kwa ufadhili wa Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB).

Nao baadhi ya wafanyabiashara mkoani Shinyanga waliiomba serikali kuendeleza ujenzi wa uwanja huo wa ndege ili kuanza kuwahudumia wasafiri kutoka mkoani humo na kuondokana adha ya kusafiri kuelekea mkoani Mwanza ili kupata usafiri wa ndege.

# Kampuni madini kutoa elimu athari matumizi ya plastiki

**Na Mwandishi Wetu,** SENGEREMA

KAMPUNI ya Sotta Mining Corporation Limited ambayo ni mwendelezaji wa mradi wa dhahabu wa Nyanzaga imesema katika kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani itatoa elimu ya athari zitokanazo na plastiki kwenye mazingira, kwa afya ya binadamu pamoja na wanyama.

Pia imesema inajivunia kuendelea kuunga mkono maadhimisho ya siku hiyo kwa kushirikiana na wakazi wa Mji wa Ngoma.

Meneja Mkuu na Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Damien Valente, aliyasema hayo katika taarifa yake kwa vyombo vya habari.

Alisema katika kuadhimisha miaka 50 tangu kuanzishwa kwa Siku ya Mazingira Duniani na kwa kuzingatia kauli mbiu ya mwaka huu isemayo 'suluhisho la taka za plastiki' wataendesha shughuli mbalimbali kwenye jamii kwa lengo la kueneza ufahamu wa athari zitokanazo na plastiki kwenye mazingira.

Alisema wataendelea kujizatiti kuzingatia kanuni za kulinda mazingira zinazokubalika ulimwenguni wakati wa utekelezaji wa shughuli za mradi kwa kupunguza madhara yatokanayo na shughuli zake.

Damien alisema katika wataendelea kuboresha ufanisi katika utunzaji wa mazingira wakati wa utekelezaji wa shughuli za mradi ili kuhakikisha mazingira bora kwa jamii inayozunguka maeneo ya mradi.

"Sina budi kuwapongeza wafanyakazi wenzangu kwa kuyafanya maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Mazingira kuwa yenye mafanikio. OreCorp pamoja na Sotta Mining zinajizatiti kulinda mazingira, ambayo ni kipaumbele na hilo linadhihirishwa kila siku na kila mmoja aliyehusika katika kuendelea kuujenga mradi wa dhahabu wa Nyanzaga. Kila siku ni siku ya mazingira kwa Kampuni ya Sotta."

SMCL ni mradi wa pamoja kati ya serikali ya Tanzania inayomiliki asilimia 16 na kampuni ya uchimbaji madini ya Nyanzaga (84%) ambayo ni kampuni tanzu ya OreCorp Tanzania Limited kwa ajili ya kujenga mradi wa Sh. trilioni 1.1 kusini mwa Ngoma katika Wilaya ya Sengerema.

Mradi huo unatazamiwa kuwa mradi mkubwa zaidi wa dhahabu kuwahi kujengwa Tanzania ndani ya kipindi cha zaidi muongo mmoja na mradi mkubwa zaidi kuwahi kujengwa wilayani Sengerema.

Mradi wa dhahabu wa Nyanzaga upo Wilaya ya Sengerema iliyopo mkoani Mwanza kwenye ukanda wa dhahabu wa Ziwa Victoria.

Mradi huo utakapokamilika utazalisha wakia 200,000 (tani sita) za dhahabu kila mwaka kwa miaka 12 ya mwanzo na ujenzi wake utagharimu Sh. trilioni 1.1.



Ukurasa 12

MIAKA 60 AFRIKA

**Ni kama hakuna tena matumaini kumejaa hofu, vita na kukata tamaa**



Ukurasa 13

BAHARI YACHAFUKA TLP

Mwenyekiti wa Vijana Vs Katibu Mkuu, uchaguzi sasa ni ndoto



Ukurasa 14

**RECEP TAYYIP ERDOGAN:**

**'Dikteta' aliyeshinda kwenye marudio ya uchaguzi Uturuki**

siasa

JUMATANO JUNI 7, 2023

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

KADA ALI KARUME

# Anyooshewa kidole, Mwinyi aelekeza wavunja miiko CCM washughulikiwe

• Hofu ni kuepuka yaliyowahi kutokea zamani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MVUTANO unanukia katika siasa za visiwani, huku hatima ya Balozi Ali Karume, mtoto wa mwasisi wa Serikali ya Mapinduzi (SMZ), Sheikh Abeid Amani Karume, akiibua mshangao baada ya kuzusha hoja zenye masuala mengi yenye utata.

Mjadala unaoibuliwa na Ali Karume, unasababisha mvutano wa maneno kwa makada wa chama wengine wakitaka aitwe na Kamati ya Maadili ya CCM kuhojiwa, kuhusu madai kuwa haijashinda chaguzi za vyama vingi kutokana na kusimamisha wagombea ambao si chaguo la wana CCM.

Balozi Karume anawaambia waandishi wa habari visiwani hapa nyumbani kwake Maisara hivi karibuni kuwa CCM imekua ikiteua mgombea badala ya kuchaguliwa na wanachama jambo ambalo linadumaza demokrasia ndani ya chama hicho na kukwamisha ushindi.

Baada ya kauli hiyo ya Balozi Ali Karume, wanaouguswa kwanza ni kada wa CCM Mwinyi Jamali Ramadhan, anayejitokeza katika mkutano wake na wanahabari akidai kuwa maneno ya Balozi hayana msingi na yanapotosha ukweli wa upatikanaji wa mgombea wa urais wa Zanzibar katika mchakato wa chama.

Anasema uchaguzi wa kumpata mgombea umekuwa ukifanyika kwa uwazi kuliko vyama vyote vya Zanzibar na kutoa mfano wa uchaguzi wa mwaka 2020 ambako zoezi hilo lilikuwa la wazi na kila mgombea kukabidhiwa kura zake.

Anasema Balozi Karume anapaswa kuhojiwa katika kamati ya maadili kutokana na kauli anazozitoa kwa vile hazisaidia kujenga umoja na mshikamano ndani ya chama.

Anaongeza kuwa kama alikuwa anajambo la kukishauri chama alipaswa kutumia taratibu na sio kwenda kukipaka matope hadharini.



Balozi Ali Karume. **PICHA: MTANDAO**

Mambo hayakuishia hapo, Naibu Katibu wa Idara ya Uenezi Idara ya Itikadi, Uenezi na Habari wa CCM, Mbeto Khamis Mbeto, analazimika kuitisha mkutano wa wanahabari na kumlaumu Balozi Ali Karume kuwa amepotea njia na hakupaswa kusema kauli hiyo.

Anasema uchaguzi wa mwaka 2020 wanachama wa CCM zaidi ya 20 walijitokeza kugombea urais wa Zanzibar na mchakato wa kumpata mgombea ulizingatia katiba na kanuni za chama.

Anakumbusha kuwa kati ya wagombea hao, mchujo ulifanyika na hatimaye wakapatikana wanachama watano na majina yao kuwasilishwa Kamati Kuu ya CCM na baadaye matatu yalipelekwa katika mkutano wa Halmashauri Kuu na kupatikana jina moja kwa ajili ya kupeperusha bendera ya CCM katika uchaguzi mkuu.

"Wagombea watano walipelekwa Kamati Kuu badala ya kujadaliwa na Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya Zanzibar iliwapendekeza Dk. Khalid Salum Muhammed, Shamsi Vuai Nahodha, Profesa Makame Mbarawa, Khamis Mussa na Dk. Hussen Ali Mwinyi," anasema.

Anaongeza kuwa majina hayo yalichunjwa na kubakia matatu katika kikao halali cha Kamati Kuu na ndiyo yaliyopigiwa kura ya wazi akiwamo Dk. Khalid Salum, Shamsi Vuai Nahodha na Dk. Hussein Ali Mwinyi na wajumbe wa Halmashauri Kuu Taifa ya chama hicho.

Mbeto anamwambia Karume kuwa kwa mujibu wa miiko na maadili ya CCM, mwanachama yeyote kama ana jambo lake anapaswa kuliwasilisha katika chama kupitia vikao halali viwe vya shina, tawi, jimbo au taifa badala ya kuzungumza hadharani mambo yasiyokuwa na ukweli.

Mbeto anahoji, "Balozi Karume anatambua taratibu za uchaguzi na kama uchaguzi wa Zanzibar wa mwaka 2015 ulifanyika mara mbili kwa nini alikubali kuteuliwa waziri wa SMZ kama haukuwa huru na haki?"

"Balozi Karume ni mwanachama wetu kama anahisi ana ushauri wowote kwa chama milango ipo wazi kusema ndani ya vikao halali vya chama badala ya kuropoka nje ya taratibu zetu,"anasema Mbeto.

**ANAVUNJA MIIKO**

Makamu wa CCM Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, anasema baadhi ya wanachama wa chama hicho wanavunja maadili hawachukuliwi hatua na kwamba huo

INAENDELEA UK. 12

# Ni kama hakuna tena matumaini kumejaa hofu, vita na kukata tamaa



Wakimbizi wa Afrika wakizama baharini kukimbilia Ulaya ili kukwepa shida kwenye nchi zao. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

MATAIFA ya Afrika Kusini ya Jangwa la Sahara yanakabiliwa na hali mbaya ya uchumi na hata maisha ya raia wake ni hoi.

Katika kipindi hiki inaposherehekea miaka 60 ya Umoja wa Afrika OAU ulioanzishwa Mei 1963, lakini sasa ni African Union (AU) eneo la Kusini ya Sahara limejaa vita vya wenyewe kwa wenyewe, hali ya kuyumba kisiasa, mdororo wa uchumi unaotokana na bei za malighafi zinauzwa nje kuzidi kupungua mfano madini, mazao ya kilimo na maliasili.

Hali si ya kuridhisha na mataifa mengi yana madeni makubwa yanayotokana na pesa za miradi ya maendeleo kubakia kuwa mikopo mikubwa inayotoka kwenye taasisi za fedha kama WB, IMF, mataifa mbalimbali kama China na India.

**MIONGO YA VITA**

Wakati mwezi uliopita Afrika ilijigamba kwa kukua kwa 'kimo na kimwili' ikisherehekea miaka 60 migogoro ya silaha inatishia uwezekano wa programu zinazolenga ukuaji wa uchumi na kuondoka kwenye umaskini.

Tatizo sugu la vita mfano Congo DRC, Somalia, Sudan, Sudan Kusini, Jamhuri ya Afrika ya Kati (CAR) na eneo lote la Sahel linazidi.

> Katika maamuzi ya pamoja ya mkutano wa kilele wa ICGLR msisitizo wa maamuzi ya Mkutano mdogo wa Kilele wa Amani na Usalama mashariki mwa DRC uliofanyika Novemba 2022.

Mwezi Juni unaanza kwa mkutano wa 10 wa Dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Nchi za Maziwa Makuu (ICGLR) uliofanyika jijini Luanda, Angola Jumamosi iliyopita.

Kikao hicho cha dharura kinatanguliwa na Mkutano wa mawaziri uliofanyika Juni 2, 2023 unaojadili na kuangalia hali ya amani na usalama katika Ukanda wa Maziwa Makuu hasa katika nchi za Jamhuri ya Sudan na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Angola ndiyo inayoitisha mkutano huo, Rais na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu (ICGLR) ni Joao Manuel Lourenco, anayefanya hivyo kutekeleza maazimio ya Mkutano wa 16 wa Dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanyika Mei 2022 jijini Malabo, Equatorial Guinea.

Viongozi wa eneo hilo wameiomba Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kuharakisha mchakato wa kuyapokonya makundi yote yenye silaha katika eneo la mashariki mwa nchi hiyo kama sehemu ya sharti muhimu la kusuluhisha mzozo wa mashariki mwa DR Congo.

Wakati kuna zaidi ya vikundi 130 vyenye silaha vya DRC na vya kigeni vilivyoko mashariki mwa Congo, wageni ni pamoja na FDLR, wanaoelezwa kuwa wanamgambo wa mauaji ya halaiki, wanaoundwa na mabaki ya watuhumiwa wa mauaji ya kimbari ya 1994 ya Rwanda.

Yalifanywa dhidi ya Watutsi nchini Rwanda, FDLR sasa imejiunga na jeshi la taifa la DRCongo (FARDC).

Mkutano wa ICGLR unahimiza nchi hiyo kuharakisha utekelezaji wa Mpango wa Upokonyaji Silaha, Uondoaji, Uunganishaji na Uimarishaji wa Jamii wa waasi wanaobadilika hatua muhimu kwenye utatuzi wa mzozo wa mashariki mwa DRC.

Katika maamuzi ya pamoja ya mkutano wa kilele wa ICGLR msisitizo wa maamuzi ya Mkutano mdogo wa Kilele wa Amani na Usalama mashariki mwa DRC uliofanyika Novemba 2022.

Ulitarajiwa kufikia sasa FDLR wawe wamepokonywa silaha na kurejesha makwao bila masharti, lakini hadi sasa, hakuna hatua iliyochukuliwa na serikali ya DRC.

Mkutano wa wiki iliyopita wa ICGLR unasisitiza kutekeleza maamuzi ya mkutano mwingine mdogo uliofanyika Februari mwaka huu Ethiopia.

Ndiyo uliobainisha kuwapo wakimbizi 80,000 wa DRC nchini Rwanda na hitaji la dharura la kurejeshwa nyumbani kwao salama.

Kati ya wakimbizi 80,000 nchini Rwanda, kuna wanaoelezwa kuishi makambini kwa zaidi ya miaka 25. Hali imekuwa mbaya hivi karibuni huku wakimbizi zaidi wa Congo wakiendelea kukimbilia Rwanda kutokana na mapigano hasa ya waasi wa M23 na muungano wa serikali unaojumuisha wanamgambo wenye silaha kama FDLR.

ICGLR pia unawaagiza Mawaziri wa Mambo ya Nje wa Angola, Congo, Rwanda na Burundi kukutana mara kwa mara na kutathmini kwa pamoja hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa mpango wa Luanda na Mpango wa Utekelezaji wa Pamoja wa Bahari ya Pasifiki ya Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, pamoja na kuhalalisha uhusiano wa kisiasa na kidiplomasia kati ya Rwanda na Congo.

Ukiangalia hali hiyo ya Congo, ni wazi kuwa jumuiya za kimataifa kuanzia Umoja wa Mataifa UN, AU Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS), Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) Umoja wa Ulaya na Marekani zote kwa nyakati tofauti zimetafuta njia za kusaidia mataifa yenye migogoro kuacha vita lakini bado vinaendelea kupiganwa.

Taasisi na nchi zimehusika katika operesheni za ulinzi wa amani kwa mfano UN -DRC imekuwa na majeshi ya MONOSCO, vikosi vya Jumuiya ya Afrika Mashariki vimekuwa ikifanyakazi DRC na hata Nigeria nchini Sierra Leone.

Mashirika kama vile Benki ya Dunia na IMF pia yanasaidia nchi zinazotoka katika migogoro ya silaha kujenga upya miundombinu na kuboresha uwezo wao wa kukusanya kodi na kutoa huduma muhimu za kijamii.

Lakini DRC na Afrika nzima hali itaendelea hivi mpaka lini? Ni miaka 60 ya uhuru lakini bado ni maskini, kunanuka vita, njaa, demokrasia duni na hakuna hatima.

Mpango wa Benki ya Dunia na IMF ulioimarishwa wa Nchi Maskini Zenye Madeni Mengi (HIPC) uliolenga kutoa unafuu wa madeni wa haraka zaidi, wa kina na mpana zaidi kwa nchi nyingi kama 30, hasa katika Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara haukusaidia mataifa mengi.

Leo hali inazidi kuwa duni, kiuchumi, huduma za jamii, uhasamana madeni makubwa na umaskini unaongezeka.

Ndiyo maana watu wanasema Afrika itahitaji kuumbwa upya lakini kwa hii iliyokuwapo ni kitendawili kisicho na majibu.

## Anyooshewa kidole, Mwinyi aelekeza wavunja miiko washughulikiwe

**INATOKA UK. 11**

siyo utaratibu na kutaka watu hao washughulikiwe haraka kwa mujibu wa taratibu za chama.

Rais wa Zanzibar anasema haiwezekani wanachama wanaovunja maadili wanaachiwa hivyo akazitaka kamati za maadili kutekeleza wajibu wao kwasababu haiwezekani mwanaCCM kusema maneno ya ovyo dhidi ya chama na kuwatukana viongozi wa juu.

Anaonya kuwa hali hiyo itapelekea kutengeneza makundi hivyo ni vyema kuitwa na kukanywa ili wajirekebishe na wasiotaka kujirekebisha hatua stahiki zichukuliwe mapema.

"Tukiyafanya haya chama chetu kitakuwa na nguvu na wala hakitoweza kushindwa na chama chochote tusitengeneze ugomvi ndani ya chama, hakuna uhai kama hakutakuwa na umoja na mshikamano nawataka wanachama kuwa wamoja."

Rais Mwinyi anawataka wanachama kuvunja makundi ili chama kuwa na umoja katika kukiendesha na kuondosha tofauti zao na kwamba hilo litawasaidia kuhakikisha adui hayumo katika chama na jukumu libaki kupambana na maadui wa nje.

Wanachama wa CCM ambao wamewahi kuvuliwa uwanachama kwa kwenda kinyume na miiko ni Maalim Seif Sharif Hamad, Mawaziri; Hassan Nassoro Moyo, Mansour Yussuf Himidi wa SMZ (wote ni marehemu) mwingine ni mwanasiasa mkongwe Baraka Shamte kabla ya kurudishiwa uanachama pamoja na aliyekuwa mwakilishi wa jimbo la Jang'ombe, Abdallah Maulid Diwani.

BAHARI YACHAFUKA TLP

# Mwenyekiti wa Vijana Vs Katibu Mkuu, uchaguzi sasa ndoto

**Na Sabato Kasika**

• Ofisi ya Msajili yaishangaa, mchambuzi siasa awapasha



Mwenyekiti wa Vijana wa TLP Taifa, Aivan Maganza, alipotangaza tarehe ya uchaguzi wa mwenyekiti wa TLP taifa.



Katibu Mkuu wa TLP akitangaza kumfukuza uanachama Aivana Maganza kwa utovu wa nidhamu. **PICHA: SABATO KASIKA**

MIGOGORO ya kiuongozi imekuwa na sehemu ya vyama vya siasa, kiasi kwamba inasababisha baadhi yake visifanye shughuli za kisiasa kwa kusuasua na vingine kujikuta vikifa kifo cha kawaida.

Baadhi ya vyama ambako sasa ni kaa la moto licha ya kuruhusiwa kufanya shughuli za kisiasa kwa amani japo milango imefunguliwa ni pamoja NCCR-Mageuzi ambako baadhi ya wanachama wakiongozwa na Joseph Selasini, wamemwondoa kwenye chama Mwenyekiti James Mbatia. Kadhalika ndani ya CUF kumekuwa na mgogoro wa miaka kadhaa wa kiuongozi na baadhi ya wanachama wametimuliwa, lakini kiini ni kutofautiana na uongozi wa juu.

Na hivi karibuni ni Chama cha Tanzania Labour Party (TLP), kimeingia katika mgogoro wa kiuongozi ambao huenda usipate suluhu iwapo viongozi hawatakaa meza moja kuumaliza.

Heka heka zilianza wiki iliyopita, Katibu Mkuu wa TLP, Richard Lyimo, alitangaza kumfukuza uanachama Mwenyekiti Vijana Taifa, Aivan Maganza, lakini naye hakukaa kimya akamjibu mwenyekiti na kusema kamati ambayo katibu ameitumia kumvua uanachama, haipo miaka mingi iliyopita na kwamba hata kama ingekuwapo haina uwezo huo, moto unaendelea kufukuta na hema la TLP linawaka moto.

Kutokana na hali hiyo, Nipashe inazungumza na mchambuzi wa siasa, Abbas Mwalimu, ambaye anaelezea sababu za migogoro hiyo na kusema zipo nyingi mojawapo ikiwa ni viongozi kuwa miungu watu.

"Chama kinaanzishwa, kiongozi ni huyo huyo, kutokuwapo kwa uwazi, wanachama wanachangishwa fedha bila kuambiwa zinatakiwa kutumika kwa ajili ya nini, hawatakiwi kutoa maoni, hali haiwezi kuwa shwari," anaeleza Mwalimu.

Mchambuzi huyo anaongeza kuwa vyama kukosa itikadi ni sababu nyingine ya kuibua migogoro, ubadhirifu wa fedha na hata rushwa ikiwamo ya ngono wakati wa uchaguzi ndani ya vyama hivyo huleta migogoro mingi.

"Vilevile katiba ya vyama haiainishi mipaka ya kiuongozi na taratibu, kwani vyama vingine huwezi kujua ni nani msemaji wa chama na sababu nyingine ni kwamba havina mifumo ya kuzuia migogoro," anasema Mwalimu akivitaka vijitafute na kujirekebisha.

Anafafanua kuwa vyama vingi vina viongozi imara, lakini havina mifumo imara na kwamba matokeo wakati wa kujadili jambo badala ya kutumia mfumo, yanazingatiwa matakwa ya kiongozi na kusababisha migogoro.

**TLP INAVYOTEKETEA**

Kwa sasa kuna kila dalili za kuibuka mgogoro wa kudumu baada ya Katibu Mkuu Richard Lyimo, naye kutangaza kumfuta uanachama Mwenyekiti wa Vijana Taifa, Aivan Maganza, mwishoni mwa wiki katika mkutano na wanahabari, jijini Dar es Salaam akielezea kuwa umekutwa na kosa na utovu wa nidhamu.

> Pamoja na mambo mengine, mwenyekiti huyo wa vijana anatuhumiwa kutangaza tarehe ya uchaguzi wa mwenyekiti wa chama taifa kuwa ni Juni 18 mwaka huu bila baraka za chama.

Katika maelezo yake, anasema kamati ya nidhamu ya chama hicho taifa ndio iliochukua uamuzi huo baada ya kumkuta na kosa hilo, kwa kuitisha mkutano huo na kuwakashifu viongozi wa chama hicho.

"Pamoja na mambo mengine, mwenyekiti huyo wa vijana anatuhumiwa kutangaza tarehe ya uchaguzi wa mwenyekiti wa chama taifa kuwa ni Juni 18 mwaka huu bila baraka za chama," anasema Lyimo.

"Pamoja na mambo mengine, mwenyekiti huyo wa vijana anatuhumiwa kutangaza tarehe ya uchaguzi wa mwenyekiti wa chama taifa kuwa ni Juni 18 mwaka huu bila baraka za chama," anasema Lyimo.

Anafafanua kuwa kamati hiyo ilikutana na kupendekeza kwenye kikao cha sekretarieti ya chama kwamba hafai kuwa kiongozi wa TLP katika ngazi yoyote akiongeza:"Kikao cha sekretarieti nacho kwa idhini ambayo kimepewa na Katiba ya TLP kwa kauli moja kinamfukuza katika chama," anasema.

Katibu huyo anaeleza kuwa Maganza haruhusiwi kufanya au kuonekana katika ofisi yoyote ya TLP kuanzia ngazi ya taifa hadi shina, na kwamba anaruhusiwa kukata rufani kwa ngazi za juu zaidi za chama.

Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa inasema haijasikia mgogoro huo wa kufukuzana na inashangaa kwa nini unaibuka wakati ikiendelea kushughulikia malalamiko yaliyomo ndani ya chama.

Msajili Msaidizi wa Vyama vya Siasa, Sisty Nyahoza anasema wiki chache zilizopita, alipokea malalamiko toka kwa baadhi ya wanachama wa TLP ambao anataka uchaguzi ufanyike haraka na kwamba ofisi inaendelea kuyashughulikia.

"Mwenyekiti wa vijana TLP kufukuzwa uanachama, ninasikia kwako, pia ninashangaa kwa nini inakuwa hivyo, kwani tunaendelea kushughulikia malalamiko yao, wanaibua mgogoro mwingine," anasema.

**AJIBU MAPIGO**

Baada ya hatua hiyo, Maganza anasema katibu mkuu hawezi kutoa maamuzi kwa jambo ambalo ana masilahi nalo na kwamba ni mgombea na nafasi ya mwenyekiti wa chama taifa kama ilivyo yeye Maganza.

Anasema kikao cha kikatiba cha kumvua uanachama kiongozi wa kitaifa ni mkutano mkuu taifa, kikao cha kumsimamisha uongozi kiongozi, ni halmashauri kuu taifa lakini haina mamlaka kumvua uanachama.

"Kamati ya nidhamu kazi yake ni kutoa mapendekezo kwa halmashauri kuu au kamati kuu, haina mamlaka kutoa adhabu, mkutano mkuu wa taifa ndio unaoweza kumvua uanachama kiongozi wa kitaifa," anasema.

Anafafanua kuwa Katiba ya TLP katika ibara ya 18: 3 (p), inaeleza kuwa kazi za mkutano mkuu Taifa unaweza kumvua uanachama au uongozi au kiongozi yeyote pamoja na mwenyekiti taifa iwapo itadhihirika anakiuka kuwa anavunja katiba na maadili ya chama.

"Ibara ya 18:5 (k), kazi ya halmashauri kuu ya taifa ni kuandaa mkutano mkuu wa taifa kifungu I, kushauri au kuunda kamati au tume kwa shughuli maalum," anasema.

Anaongeza kuwa katika ibara ya 26:11, inaeleza kuwa kutakuwa na kamati ya nidhamu taifa ambayo mwenyekiti wake pamoja na wajumbe wake watateuliwa na mwenyekiti taifa wa chama.

Maganza anasema kwa muda mrefu TLP haina kamati hiyo, tangu wakati wa uhai wa Mrema, ambapo anashangaa kusikia kuwapo kwa kamati hiyo wakati chama hakina mwenyekiti mwenye mamlaka ya kuiteua.

"Ibara ya 26:13 inaeleza kazi za kamati hiyo katika kifungu (b) kuwa kutoa mapendekezo kwa vikao vinavyohusika kwa hatua zaidi, hivyo hakuna sehemu kamati ya nidhamu inaweza kutoa adhabu.

Anasema kuwa kama kamati hiyo ingekuwapo, ingemuita na kumhoji na kutoa na mapendekezo, na kwamba hakuitwa, badala yake amesikia tu kwamba amefukuzwa katika chama.

"Taarifa niliotoa kwa waandishi wa habari kuhusu tarehe ya uchaguzi na kusababisha uamuzi uliotangazwa na katibu mkuu, iko kama ilivyo, asipokuwa makini ndiye atafukuzwa uanachama, siyo mimi," anasema.

Maganza anasema viongozi wote wa makao makuu ya chama ambao kuanzia vitengo vya vijana, akina mama na wazee na Mkutano Mkuu Halmashauri Kuu, Machi tano walikubaliana kwamba uchaguzi wa mwenyekiti wa TLP taifa ufanyike Juni 18, 2023.

"Pamoja na uchaguzi huo, kutakuwa na mkutano mkuu wa mwaka wa chama chetu, taarifa iwafikie wajumbe wa mkutano mkuu TLP taifa popote walipo kwamba chama makao makuu kwa kushirikiana na idara tutaandaa utaratibu wote, na tayari maandalizi yanaendelea," anasema.

Mgogoro ndani ya TLP ulianza Machi mwaka huu baada ya uchaguzi wa mwenyekiti wa chama hicho taifa kuahirishwa ghafla na kusababisha sintofahamu inayoendelea hadi kufikia kufukuzana.

Uchaguzi huo ulikuwa ufanyike ili kuziba nafasi iliyoachwa wazi na aliyekuwa mwenyekiti wa chama hicho taifa, Augustine Mrema, aliyefariki dunia Agosti mwaka jana.

RECEP TAYYIP ERDOGAN:

# ‘Dikteta’ aliyeshinda kwenye marudio ya uchaguzi Uturuki

• Ni ‘popo’ mshirika NATO, Russia, Ukraine na Ulaya

**Na Ani Jozeni**

USHINDI wa Rais Recep Tayyip Erdogan (69) wa Uturuki katika duru ya pili ya uchaguzi wa rais haikuwa hali ya kushangaza. Lakini ukweli unabakia kuwa mambo hayakuwa rahisi ndiyo maana katika raundi ya kwanza ya kura zilizopigwa Mei 14, alipata asilimia 49.5 wakati mpinzani wake wa karibu Kemal Kilicdaroglu akiibuka na asilimia 44.9, wakiwa wanakaribiana.

La ajabu ni jinsi ambavyo matokeo ya awamu ya pili yaliendana bila hitilafu na mtawanyiko mpya wa kura baada ya ushindi usiotosha kwake kupatikana katika awamu ya kwanza. Alipata takriban asilimia 49 awali, halafu akafikia asilimia 52.5, wakati wa kupiga kura za marudio.

Kemal Kılıçdaroğu, mshindani wake mkuu alipata asilimia 43.12 na Sinan Oğn akaambulia asilimia 5.2 halafu akajitoa siku chache kabla ya kura kupigwa, Tume ya Uchaguzi ikatangaza kuwa kura zake zitahesabiwa.

Ina maana ya kufahamu ni sehemu kubwa kiasi gani ya wapigakura ilikuwa na imani naye na siyo matumaini ya kuvuna chochote cha ziada. Ukiangalia matokeo ya duru ya pili unapata picha kuwa wafuasi wake waligawanyika sehemu mbili zinazofanana, ila zaidi walirudi kwa Erdogan. Hawakutaka kumuunga mkono mgombea wa upinzani aliyebaki, kama wanavyoshauri wengi.

Kati ya asilimia tano hizo za kura baadhi walimwongozea Erdogan kura zao akapata takriban asilimia 3.3 zaidi ya zile za awali, huku mpinzani wake akipata unafuu wa asilimia nyingine tatu kupanda kutoka asilimia 44 hadi 47.8.

Hesabu hizo haziendani moja kwa moja na ile asilimia tano ila ilikuwa asilimia 5.2 na kulikuwa na asilimia 0.4 iliyoendana na ya awali kwa

Muharrem ğnce. Hapakuwa na ubabaishaji katika kuhesabu kura, hilo ndilo la kujifunza.

Ni kielelezo cha ‘uimla’ wa kiongozi huyo ambaye inavyoelekea anahakikisha kuwa mifumo wa kuhabarisha ya dola iko upande wake au inaongozwa na wafuasi wake.

Na anafahamu kuwa wengi nchini humo wanaunga mkono mwelekeo wake wa ‘uzalendo wa wastani,’ unaompa uhuru kuwa miongomi mwa nchi za Umoja wa Kujihami wa Nchi za Magharibi (NATO) na mshirika mwandamizi wa mahasimu wakuu wa NATO, Russia, China na Iran.

Sababu ni kuwa kila nchi inataka kuwa na washirika, hata kama marafiki hao ‘wanakula’ na mahasimu wao, kama ilivyo kwa nchi nyingi za Afrika.

Si rahisi kusema nini kingebadilika endapo Erdogan asingeshinda uchaguzi kwa hapa kuwapo na uwezekano wa mpinzani wake kufikia asilimia 50.



Recep Tayyip Erdogan

> Jeshi la ardhini lina usomi hafifu zaidi, na hivyo ni rahisi kuathiriwa na mihemko ya kimapinduzi inayochochea harakati zikiwamo za waasi, za kujitenga na hata zinazoanzishwa na mamluki.



Mpinzani mkuu, Kemal Kilicdaroglu. **PICHA ZOTE: REUTERS**

Siasa za Uturuki kama la ukanda wote wa Asia ya Magharibi ni mvutano kati ya hadi inayopendwa na tabaka la wakulima na viongozi wa dini lililosheheni uhafidhina halafu kuna tabaka la kibwanyenye na kisomi ambalo huendana na mageuzi au ‘utandawazi.’

Ndiyo historia ya Uturuki tangu mwisho wa vita vikuu vya kwanza karne iliyopita ambako himaya ya Ottoman ya masultani wa jadi ilisambaratishwa.

Ni hapo ambako Uturuki ilizaliwa, chini ya uongozi wa Baba wa Taifa Jenerali Mustafa Kemal Attaturk, akiongoza wimbi la vijana waliotaka Uturuki izaliwe upya, na ijitahidi ifikie viwango ya maendeleo vya nchi za Magharibi.

Siyo kwamba itikadi za kiharakati za wafuasi wa tabaka la kidini ziliisha lakini hazijawahi kuwa na nguvu katika mfumo wa siasa wa nchi hiyo licha ya misukosuko ya kubadilisha mwelekeo wa nchi kila mara.

Hata wapinzani wake hawajionyeshi waziwazi kuwa na itikadi ya jadi ya mapinduzi ya kidini kama ilivyo kwa Iran ambaye ni jirani ila Erdogan alipata mtihani mkubwa kwa kuzuka kwa jeshi la kiharamia nchini Iraq lililoua, hasa kwa kuchinja, maelfu ya watu waliokuwa katika nchi hizo mbili kwa kuulizwa maswali rahisi kuhusu imani yao halafu wakashindwa kujibu.

Uturuki haiangaiki ni serikali gani itawale huko mradi isizuke serikali inayosaidia harakati za Wakurdi nchini humo. Ni tatizo sugu la ukanda huo linalogusa Iran, Uturuki na Iraq ambalo Wakurdi wana serikali ya jimbo.

Wakati huo, kabla wimbi la ‘Dola ya Kiislamu’ halijabamizwa na kuishilia au kudumazwa katika miaka ya karibuni hasa alipoingia madarakani Rais Donald Trump nchini Marekani, Erdogan alilazimika kufanya kampeni kubwa ya ‘safisha safisha’ ya jeshi la Uturuki kuondoa wafuasi wa ‘Dola ya Kiislamu,’ kwani kuna baadhi ya viongozi wa kidini walikuwa wanafurahia wimbi hilo. Ilitangazwa kuwa uasi wa kijeshi wa kutaka kuipindua serikali ya Uturuki uligunduliwa katika Jeshi la Anga. hivyo kusafisha kulianzia huko.

‘Waliosoma Cuba’ wanajua kuwa endapo kulikuwa na hatari halisi ya jeshi la Uturuki kutaka mwelekeo wa ‘Dola ya Kiislamu’ wimbi hilo lingeanzia katika jeshi la ardhini na siyo la anga. Sababu ni kuwa wanajeshi wa anga kwa kawaida wamesheheni wasomi, hivyo wana mwelekeo wa kimageuzi.

Jeshi la ardhini lina usomi hafifu zaidi, na hivyo ni rahisi kuathiriwa na mihemko ya kimapinduzi inayochochea harakati zikiwamo za waasi, za kujitenga na hata zinazoanzishwa na mamluki.

Erdogan anashinda mapambano hayo ya mwaka 2017 na hadi wakati huu wapo wengi wanaoamini kuwa alichosema kilikuwa sahihi. Ni hali ambayo itakuwa imemsaidia katika kura kwani wananchi wanaambiwa wachague kati ya msimamizi mzalendo anayetetea uhuru wa nchi, ila akiwaacha wananchi kuwa huru na kufanya wanalotaka, Uturuki ibaki na sura yake ya kimagharibi.

Wapinzani wake siyo wana-Dola ya Kiislamu ila makundi ya mwelekeo huo yanaweza kujificha na kukwamisha mwelekeo wa kimagharibi endapo wangeshinda kiti cha urais.

Ni hali kama ya Misri, Tunisia, Iraq au Pakistan, kuwa ikipigwa kura ya wazi bila vizuizi ni wafuasi wa viongozi wa kidini ndiyo watakaoshinda, hivyo inaundwa mifumo ya kiimla ya kuzuia wasijieleze au kujipanga, wapatikane wawakilishi wanaokubalika kwa mfumo wa wastani (moderate) , huo ndiyo ‘udikteta’ wa Erdogan.





## Wananchi milioni 3 kunufaika uzalishaji hewa ya ukaa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WANANCHI zaidi ya milioni tatu nchini wanatarajia kunufaika na hewa ya ukaa inayotarajia kuzalishwa na Kampuni ya Livingway (URT) Limited inayotekeleza mradi wa Tabora Carbon Credit katika misitu iliopo mkoani humo.

Mradi huo wa wawekezaji wazawa unatekelezwa kwa ushirikiano wa Wakala wa Misitu Tanzania (TFS ) ili kuhakikisha misitu inaendelea kuwa salama kwa ajili ya kuiletea faida serikali na wananchi kwa ujumla.

Hayo yalisemwa jijini Dodoma juzi na Mkurugenzi wa URT, Dk. Ernest Irungu wakati akizungumza na Nipashe kuhusu faida mbalimbali zitokanazo na mradi huo ambazo zitawalenga wananchi moja kwa moja.

Dk. Irungu alisema moja ya faida kubwa ambazo wananchi watanufaika nazo ni pamoja na kupata ajira za muda na za moja moja kupitia miradi midogo ambayo itatekelezwa kupitia misitu hiyo lakini wananchi wanaweza kujiajiri wenyewe kwa kuweka mizinga ambayo itawasaidia kuvuna asali.

"Mradi huu unamanufaa makubwa sana kwa wananchi wengi watapata nafasi ya kuajiriwa kupitia miradi midogo ambayo itakelezwa lakini watajiajiri wao wenyewe," alisema Dk. Irungu.

Alisema pia kutakuwa na ufugaji wa nyuki pamoja na mnyororo wa thamani ndani yake ambao utawawezesha vikundi mbalimbali vya ushirika, watu binafsi pamoja na wao wenyewe kwenda kuweka mizinga katika misitu ambayo itakuwa imehifadhiwa na baadaye kuvuna asali.

Hata hivyo alisema wanatarajia kuvuna cubic tani bilioni 1.5 ndani ya miaka 30 ijayo ili kuhakikisha uhifadhi wa misitu unakuwa endelevu nchini ikiwamo kuwanufaisha wananchi kwa ajili ya mnyororo wa thamani.

Alifafanua kuwa malengo waliyonanyo ni makubwa na ili kufikia hatua hiyo watakuwa na menejimenti endelevu ambayo itahakikisha hawatashuka kiwango kwenye utunzaji wa misitu na mazingira ili kuwezesha uhifadhi wa misitu kuwa endelevu.

"Tutakuwa na menejimenti endelevu ambayo itakuwa ikiangalia kwa karibu namna ya utunzaji misitu kwa kushirikiana na serikali kupitia TFS, ili kuhakikisha jamii inanufaika ikiwamo kuinuka kiuchumi," alisema Dk. Irungu.

Aidha, alisema wataendelea kutoa elimu kwa jamii ya namna ya biashara ya hewa ukaa inavyofanyika pamoja na fursa zilizopo ndani yake ili waweze kuzichangamkia.

Alisema pia watakuwa na miradi endelevu ya kilimo ambayo itawanufaisha wakazi wa maeneo hayo kuendesha kilimo endelevu cha mazao ya matunda na biashara ambayo yatakuwa yakichakatwa ili kuwekwa katika mnyororo wa thamani.

# Watendaji serikali waagizwa kuzingatia sheria, kanuni

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka watendaji wa serikali kuzangatia sheria, taratibu na kanuni walizojiwekea kwenye utekelezaji wa majukumu yao ikiwamo usimamizi wa mikataba na makubaliano wanayoingia, ili kuepuka serikali kushtakiwa.

Alitoa tahadhari hiyo juzi jijini hapo alipokuwa akifungua maadhimisho ya miaka mitano tangu kuanzishwa kwa ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na uzinduzi wa mafunzo kwa mawakili wa serikali.

Alisema watendaji wanapaswa kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sheria, taratibu na kanuni ili kuepuka migogoro ambayo inaweza kuifikisha serikali mahakamani.

"Migogoro hii inaweza kusababisha kufunguliwa kesi ambazo zitaigharimu gharama kubwa badala ya fedha hizo kugharamia miradi mbalimbali inayoendelea nchini," alisema Majaliwa.

Pia alisema ili kuhakikisha kuwa serikali inaendelea kuimarisha diplomasia ya uchumi na kuendelea kujenga mazingira shindani ya kuvutia wawekezaji kwa ajili ya maendeleo Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na idara, wizara na taasisi za serikali zitumie kila fursa ya utatuzi wa migogoro kwa njia ya majadiliano.

"Hali hii itasaidia kuziondoa kesi mahakamani na kuzimaliza kabisa, faida yake ni kubwa kwa kuwa zinapunguza gharama kuokoa muda na kulinda mahusiano ya kidiplomasia. Nisisitize kuwa nchi yetu bado inahitaji wawekezaji katika kuchangia kwa haraka ukuaji wa uchumi na kuongeza pato la taifa letu,"alisema.

Aidha, aliwataka watendaji wote wa serikali kuongeza umakini na ushirikiano wanapo shughulikia masuala yanayohusu uwekezaji ili kuunga mkono jitihada zinazofanywa na serikali kujenga mazingira bora ya kuvutia uwekezaji.

Pia alizitaka taasisi zote za umma zenye mawakili wa serikali kuzingatia suala la utatuzi wa kero za wananchi ili kuepuka mrundikano wa mashauri ambayo hayana ulazima wa kuyafikisha mahakamani.

"Mawakili wa serikali ongezeni bidii, juhudi na weledi katika utendaji kazi wenu, fanyeni kazi kwa uzalendo kuweni wabunifu katika kuishauri serikali ipasavyo kuhusu mashauri yaliyopo na timizeni wajibu wenu," alisema Majaliwa.

Awali Wakili Mkuu wa Serikali, Dk. Boniphace Luhende, alisema tangu kuanzishwa kwa ofisi hiyo serikali imepata uwakilishi wa uhakika kwenye mashauri mbalimbali ambayo yamekuwa yakifunguliwa dhidi yake na kwa gharama nafuu ndani na nje ya nchi.

"Katika kipindi cha miaka mitano hadi kufikia Mei 31, 2023 ofisi imeendesha jumla ya mashauri 7,162 kati ya hayo mashauri 7,025 ni ya madai na 137 ni ya usuluhishi katika mwaka wa fedha 2022/23 hadi Aprili mwaka huu ofisi hii ilimaliza mashauri ya madai 518 na kati yake 45 yaliisha kwa majadiliano na mashauri ya usuluhishi 15 ambapo kati ya hayo sita yaliisha kwa majadiliano," alisema Dk. Luhende.

Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, alisema ofisi hiyo imeisaidia serikali kuokoa Sh. trilioni 7.57 kutokana na kumaliza mashauri yake kwa njia ya usuluhi.



Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye (kulia), akimsikiliza Mbunge wa Gairo, Ahmed Shabiby, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## SMAUJATA yaanza kampeni kuchangia chakula shuleni

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

SHUJAA wa Maendeleo na Ustawi wa Jamii Tanzania (SMAUJATA) Kata ya Manyoni mkoani Singida, wameanza kampeni ya kuhamasisha jamii kuchangia upatikanaji wa chakula shuleni ikiwa ni sehemu ya mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Makamu Mwenyekiti wa SMAUJATA wa Kata ya Tambukareli, Wallase Shechambo, akizungumza katika mkutano wa wananchi wa kata hiyo alisema suala la ukosefu wa chakula shuleni kunasababisha kuwapo kwa matukio ya ukatili wa kijinsia.

Naye Mwenyekiti wa SMAUJATA wa Kata ya Tambukareli, Hossen Kheri, alisema wameamua kuanzisha kampeni ya kuhamasisha jamii kuchangia chakula ili wanafunzi waweze kupata chakula cha mchana wanapokuwa shuleni.

Alisema katika uchunguzi wao wamebaini baadhi ya watoto wamekuwa wakifanyiwa vitendo vya ukatili kutokana na kudanganywa kwa kupewa pesa za kununulia chakula au kununuliwa na watu wenye nia mbaya na kujikuta wakinaswa katika mtego huo.

"Watoto wetu wanapokosa chakula shuleni ni rahisi kurubuniwa kwa kupewa hela kwa ajili ya kununulia chipsi na vyakula vingine, hivyo shime wazazi tujitoe kusaidia kupata chakula ili kuwanusuru kwani tukiamua jambo ili linawezekana hakuna sababu ya kuisubiri serikali kutufanyia suala hili," alisema.

Katibu wa SMAUJATA wa kata hiyo, Sara Yohana, alisema kukosekana kwa chakula kwa ajili ya wanafunzi kuna madhara makubwa kwani asilimia kubwa wanakuwa hawazingatii masomo darasani.

"Suala hili wala siyo la kuiachia serikali ni letu sote na njaa haina mtu mkubwa wala mtoto na mdogo kwani ukipita muda wa kula hata mtu mzima utakuta anakuwa kimya kwa maumivu ya njaa sembuse mtoto," alisema.

Katika tukio lingine kikosi cha SMAUJATA katika kata hiyo kiliibua tukio la watoto watatu wa familia moja ambao walikuwa wakifanyiwa vitendo vya ukatili na kushindwa kupelekwa shuleni licha ya mtoto wa kwanza kuwa na miaka 13, wa pili miaka tisa na mdogo wao akiwa na miaka saba.

Watoto hao inadaiwa tangu wazaliwe hawajawahi kupelekwa shuleni zaidi ya kuwapo nyumbani wakifanyiwa vitendo vya ukatili.

Hata Hivyo, baada ya viongozi hao wa SMAUJATA kupata taarifa hiyo walikwenda kutoa elimu kwa wazazi wa watoto hao kuhusu umuhimu wa watoto hao kupata elimu ambao walikiri kufanya makosa.

Pia walikwenda kuzungumza na Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi ya Tambukareli ambaye alikubali kuwapokea baada ya shule kufunguliwa mwezi ujao.



# Shule ya Msingi Sama yazalisha miche 700

**Na Grace Mwakalinga,**
KYELA

KLABU ya mazingira katika Shule ya Msingi Sama iliyopo Kata ya Ibanda wilayani Kyela Mkoa wa Mbeya, imezalisha miche 700 ambayo itapandwa maeneo mbalimbali wilayani hapa.

Akizungumza juzi kwenye maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani, Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Heri William, alisema miche hiyo itapandwa katika taasisi mbalimbali kwa lengo la kutunza mazingira.

Alisema hatua hiyo inalenga kuunga mkono jitihada za serikali katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi kwa kuhakikisha miti inapandwa na kutunza kama hatua moja wapo ya kukabiliana na janga la ukame.

"Wilaya ya Kyela ni miongoni mwa maeneo ambayo yana jua kali na joto hivyo katika kusaidia upatikanaji wa hewa safi, tumeanza kampeni ya upandaji miti kupitia klabu za mazingira za shule ambazo zitasaidia kutimiza adhma hiyo, hapa Sama tumepanda vitalu vya miche zaidi ya 700 ambayo tutagawa bure kwa wananchi na taasisi," alisema William.

Jenifer Prosper mwanafunzi katika Shule ya Msingi Sama alisema walimu wao waliwahamasisha kupanda miti kwa ajili ya faida ya kizazi cha sasa na baadaye.

Alisema kwa sasa wanaweza kuotesha miche ya miti katika vitalu na kwamba wanatamani kuzalisha zaidi lakini kikwazo ni vitendea kazi hivyo waliwaomba wadau kusaidia.

Kaimu Meneja wa Baraza la Mazingira Mikoa ya Nyanda za Juu, Patrick Mponda, alisema Tanzania ipo nyuma katika suala la utunzaji wa mazingira kutokana na kukithiri kwa shughuli za ukataji kiti ovyo na kuharibu uoto wa asili.

Alisema sambamba na shughuli za kibinadamu kwenye vyanzo vya maji kama vile kilimo, uchomaji mikaa na uvuvi imechangia uhaba wa maji.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Keneth Nzilano, alisema kazi ya upandaji miti litakuwa endelevu na kuwataka wananchi kuunga mkono jitihada hizo ili kutunza mazingira.

Diwani wa Kata ya Ibanda, Samson Mwakalobo alilishukuru Baraza la Mazingira kwa kuhamasisha utunzaji mazingira na kuliweka suala hilo katika ajenda yao.

Alisema pia kupitia mikutano ya hadhara kwa kushirikiana na wadau wa mazingira wataendelea kutoa elimu kuachana na matumizi ya mifuko ya plastiki ambayo kwa kiasi kikubwa inaharibu mazingira.



Baadhi ya wafanyakazi wa Mgodi wa Barrick Bulyahulu wilayani Msalala mkoani Shinyanga, wakishiriki kupanda miti katika Kitongoji cha Kakola wakati wa maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## RC ahimiza wazazi kupanda miti ya matunda kwa wingi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Antony Mtaka, ametoa rai kwa wakazi wa mkoa huo kupanda miti ya matunda kwa wingi itakayosaidia kuwapatia watoto lishe bora.

Mtaka alitoa agizo hilo alipo shiriki katika upandaji miti katika chanzo cha maji cha Mto Mkomera A, Mtaa wa Ilangamoto Halmashauri ya Mji wa Makambako ikiwa ni maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani.

"Njombe tunashida ya miti ya matunda, niwaombe sana wananchi, tupande miti ya matunda ili tuweze kuondokana na utapiamlo, ukondefu na kwashakoo, matunda yawe mengi hasa nyie watu wa Makambako mnabahati unaliona jua tofauti na Makete, pandeni michungwa, miembe na aina tofauti ya matunda," alisema Mtaka.

Mtaka aliwataka wakazi wa mkoa huu kutunza vyanzo vya maji kwa kuangalia na fursa za kiuchumi ikiwa pamoja na kuyatumia mabwawa kupanda samaki.

Naye Ofisa Mazingira wa Halmashauri ya Mji wa Makambako, Gift Kiwia, alisema ipo haja ya kuelimisha jamii kupanda miti kwa sababu usipopanda miti kunakua na upungufu wa maji lakini vile vile uchumi wa nchi utapungua.

Alisema: "Lakini sambamba na hilo tunapanda miti kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan katika kampeni mbalimbali, tunapotunza vyanzo vya maji tutaongeza nguvu hata kwenye Bwawa la Nyerere ili liweze kupata maji ya kutosha kutoka huku," alisema Kiwia.

Kiwia alisema katika kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani wamefanikiwa kupanda miti 850 aina ya mivengi.

# Wazazi Mbeya kupewa elimu matunzo ya watoto

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

ZIKIWA zimesalia siku chache kuadhimishwa Siku ya Mtoto wa Afrika Duniani, Mwenyekiti wa Vituo cha Taarifa na Maarifa, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Flora Mlowezi, amesema miongoni mwa ajenda katika maadhimisho hayo ni kutoa elimu kwa wazazi kuacha tabia ya kujielekeza zaidi kwenye shughuli za kiuchumi na kusahau jukumu la kuwahudumia watoto.

Alisema jambo hilo limechangia kwa kiasi kikubwa vitendo vya ukatili wa kijinsia ikiwamo ulawiti na ubakaji dhidi ya watoto.

Aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na Nipashe juu ya maoni yake kuelekea maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika Duniani yanayoadhimishwa kila mwaka Juni 16.

Alisema vitendo vya ukatili kwa sasa vimeshamiri kwa sababu wazazi hususani wanawake wamejikita zaidi kwenye shughuli za kutafuta pesa kuliko kuwahudumia watoto ambao wanahitaji ukaribu. "Kina mama tupo bize sana kutafuta pesa kuliko kufuatilia mienendo ya watoto wetu, siyo shule wala nyumbani hatujui wana hali gani wanapitia mambo gani sisi ni pesa tu, tunasahau hizo fedha tunatafuta kwa ajili yao sasa wakibakwa au kulawitiwa tutakwenda kuzitafuta," alisema Flora.

Makamu Mwenyekiti wa SMAUJATA, Oliver Kibona, alisema wazazi wamewaachia jukumu la kulea watoto walimu hali inayosababisha kushamiri kwa vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Hivyo, aliwaasa wazazi kushirikiana na walimu kuwalea watoto ili kuwafundisha maadili mema na kuepukana na vitendo vinavyovunja maadili ya Mtanzania kama vile ushoga.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Ijombe, Angumbwike Mwalesa, alisema baadhi ya wanawake wanavunja ndoa zao kwa sababu ya kukosa elimu ya kujitambua.

Alisema wanawake wanapaswa kuwa wanyenyekevu kwa waume zao licha ya baadhi yao kuwa na kipato kikubwa ili kuwalea watoto kwa pamoja.

Hivi karibuni katika moja ya vikao vya Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Diwani wa Kata ya Ijombe, Marry Mbengele, aliiomba serikali kutoa maelekezo kwa vitendaji wa vijiji na kata kutunga na kusimamia sheria ndogo ambazo zitawabana wazazi wanaowatelekeza watoto wao.

Alisema tayari Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, imetunga sheria mbalimbali kwa ajili ya ulinzi na usalama wa mtoto kwa kuzingatia miongozi ya sheria ya haki zao kupitia katiba na mikataba ya kimataifa, lakini maeneo ya vijijini sheria hizo hazitekelezwi.

"Tunawashukuru sana wadau wetu wakiwemo Mtandao wa Jinsia nchini TGNP ambao wamekuwa karibu nasi kutujengea uwezo wa namna ya kupigania haki za watoto, wanawake na wenye ulemavu kwenye jamii yetu," alisema Marry na kuongeza:

"Elimu waliotupatia imetusaidia kupaza sauti na kuelimisha jamii kuachana na mila kandamizi ambazo zinachochea vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake, watoto na wenye ulemavu."



## Umeme wa megawati 18 kukuza uchumi wa Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema mradi wa uzalishaji wa umeme megawatti 18 unaofadhiliwa na Benki ya Dunia (WB) utasaidia upatikanaji wa vyanzo vya umeme mbadala, kurahisisha shughuli za maendeleo na ukuaji wa uchumi.

Hayo yalisemwa jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Waziri wa Maji, Nishati na Madini, Shaibu Hassan Kaduwara, wakati akitoa ufafanuzi kuhusu mikakati ya serikali katika upatikanaji wa nishati mbadala ili kukabiliana na uhaba wa umeme kwa matumizi ya shughuli za viwanda.

Alisema juhudi za kutafuta nishati mbadala ya umeme kwa ajili ya kuacha kutegemea chanzo kimoja cha umeme kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) zinaendelea kwa kutafuta vyanzo mbalimbali vya nishati hiyo.

Naibu waziri huyo alisema serikali inatekeleza mradi wa upatikanaji wa umeme megawatti 18 unaofadhiliwa na WB unaotekelezwa na Kampuni ya ZESTA ukiwa na majukumu ya upatikanaji wa nishati ya uhakika.

Alisema utekelezaji wa umeme huo utakinufaisha Kisiwa cha Pemba katika baadhi ya maeneo ikiwamo yale yanayokwenda katika miradi ya wawekezaji.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea na juhudi za kutafuta umeme mbadala ambapo Benki ya Dunia inatekeleza mradi wa megawatti 18 hatua ambayo itasaidia kwa kiasi kikubwa kuwapatia wananchi umeme zaidi katika maeneo ya vijijini," alisema.

Aidha, alisema Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) linatekeleza mradi wa usambazaji wa umeme vijijini ambao unafadhiliwa na mashirika mbalimbali ikiwamo Serikali ya Norway.

Alisema kukamilika kwa mradi huo kwa kiasi kikubwa utaviwezesha vijiji vyote vya Unguja na Pemba kupata huduma ya umeme ya uhakika.

Kadhalika, aliutaja mradi mwingine wa umeme wa jua ambao unatekelezwa katika baadhi ya maeneo ya Kisiwa cha Pemba kama vile Shamiani.

"Mheshimiwa mwenyekiti hizo ni baadhi ya sehemu za juhudi za kupata umeme mbadala na kuacha kutegemea moja kwa moja kwa chanzo kimoja cha umeme wa TANESCO kutoka Tanzania Bara," alisema.

Zanzibar inapata umeme wa uhakika kutoka TANESCO ambapo kwa upande wa Pemba kinapata umeme kutoka Mkoa wa Tanga.

# CAG agoma kujibu tuhuma zinazomkabili

**Na Mwandishi Wetu**

SIKU moja baada ya Baraza la Wawakilishi kumtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Othman Abassi Ali kuliomba radhi baraza hilo kutokana na kauli zake zilizodaiwa kulibeza na kulidharau, CAG huyo agoma kuzungumza na waandishi wa habari.

Baadhi ya waandishi wa habari jana walifika katika ofisi ya CAG iliyopo Maisara Mjini Unguja kwa ajili ya kupata kauli yake kuhusu tuhuma zinazomkabili dhidi yake lakini aligoma kuzungumza.

"Kwanza mmekuja bila ya ahadi yoyote, hivyo sitazungumza kitu kwa hili naomba mwondoke," alisema CAG.

Licha ya waandishi kufika ofisini kwake bila ya kuwa na ahadi naye lakini walimwomba kukutana nao kwa mara nyingine ili kutekeleza majukumu yao lakini alikataa.

CAG akiwasilisha ripoti yake ya mwaka 2022 kwa Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ally Mwinyi mwishoni mwa wiki, alisisitiza suala la ushirikiano kwa taasisi mbalimbali ili kupata taarifa anazozihitaji, kuonyesha dosari kwa baadhi ya taasisi kutotoa ushirikiano kwa ofisi yake.

Waandishi wa habari walifika katika ofisi ya CAG kwa ajili ya kufanya naye mahojiano walishangaa kiongozi hiyo kukataa kutoa ushirikiano ili kutekeleza majukumu yao.

"Tulifika ofisini kwake kwa ajili ya kupata kauli yake baada ya tuhuma zilizotolewa na Baraza la Wawakilishi dhidi yake, lakini amekataa kabisa kuzungumza na sisi," alisema mmoja wa waandishi hao ambaye hakutaka kutajwa jina lake.

Alisema baadhi ya viongozi hawataki kutoa ushirikiano kwa waandishi wa habari hasa pale wanapohitaji taarifa kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao.

"Dk. Mwinyi amekuwa akisisitiza kuhusu ushirikiano kwa waandishi wa habari katika kutoa taarifa lakini baadhi ya viongozi huwa wagumu hasa pale sisi tunapohitaji taarifa lakini huwa wepesi pale ambapo wanatuhitaji sisi kwa ajili ya taarifa zao zifike kwa umma," alisema.

Juzi Baraza la Wawakilishi kupitia Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali ya baraza hilo (PAC), Juma Ali Khatib, alisema mkaguzi huyo amelibeza na kudharau baraza hilo hasa kupitia kamati za kuchunguza na kudhibiti hesabu za serikali ya kwamba hazina uwezo wa kufanya kazi ripoti zake ikiwamo za TEHAMA.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa CPS, Sebastian Dietzold (wa pili kushoto), akizungumza kwenye mdahalo uliolenga kuangalia fursa zinazoweza kupatikana katika sekta ya nyumba zinazochochewa na kushamiri kwa sekta ya utalii Zanzibar, wakati wa uzinduzi wa Ofisi mpya ya CPS Masaki, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Wengine ni Meneja wa Bankable, Abdulrahman Said (kushoto), Mkurugenzi Mtendaji wa Watumishi Housing Investment, Fred Msemwa (wa pili kulia) na Mwenyekiti Mtendaji wa Hotel Association Zanzibar na Rais wa Conservation Capital, Graham Leslie. **PICHA**: **MPIGAPICHA WETU**

# DK. Mwinyi ahimiza upatikanaji majisafi na salama

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema upatikanaji wa majisafi na salama ni muhumu katika ustawi wa jamii na maendeleo ya ukuaji wa uchumi Zanzibar.

Aliyasema hayo Ikulu Zanzibar wakati akizungumza na Balozi Mdogo wa India, Zanzibar, Dk. Kumar Praveen, aliyefika kujitambulisha.

Rais Dk. Mwinyi alisema, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar bado inajivunia ushirikiano mzuri ulipo baina yake na India na kwamba Zanzibar inanufaika na fursa mbalimbali kutoka India ikiwamo masomo pamoja miradi ya maji.

Pia Dk. Mwinyi aliishukuru Serikali ya India kwa ushirikiano wanaoendelea kuutoa kwa SMZ hususani katika ufadhili wa miradi ya maji inayotekelezwa kupitia mkopo wa Benki ya Exim ya India.

Akizungumzia ujenzi wa Chuo Kikuu cha Teknolojia cha IIT, kinachotarajiwa kujengwa Zanzibar kwa Ushirikiano wa Serikali ya India, Rais Dk. Mwinyi alimweleza Balozi Praveen kwamba mazungumzo baina ya SMZ na wahadhiri kutoka Taasisi ya Teknolojia ya India yanaendelea vizuri na wapo kwenye hatua nzuri ya mpango huo kwa ajili ya utekelezaji wake.

Alisema Serikali ya Zanzibar imeridhishwa na kasi ya uanzishwaji wa taasisi hiyo kwa Zanzibar ambayo inatarajiwa kuanza Oktoba mwaka huu kwa ushirikiano wa pande mbili hizo.

Akizungumza katika hafla hiyo, Dk. Kumar Praveen, aligusia miradi ya maji Zanzibar inayofadhiliwa na Serikali ya India, mradi wa Chuo cha Ufundi wa Amali, Pemba pamoja na ufadhili wa masomo kwa watumishi wa Zanzibar nchini India. Alisema Waziri wa Mambo ya Nje ya India, Dk. Subrahmanyam Jaishankar anatarajiwa kuwasili nchini Julai mwaka huu, kwa ajili ya uzinduzi wa miradi ya maji Zanzibar, kwamba katika ujio wake huo anatarajiwa kufika jijini Dar es Salaam na Dodoma.

Uhusiano wa diplomasia uliopo baina ya Tanzania na India ni wa historia ambapo India ilifungua ubalozi wake jijini Dar es Salaam Novemba mwaka 1962 na mwaka 1974 ikafungua ubalozi mdogo Zanzibar.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTELEWA NA CHETI



**WELECELE ALBERT JOB** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0804-0081** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **D.C.T MVUMI SEKONDARI** mwaka 2013. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/MPW/RB/84307/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MARIA EMMANUEL MANDA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili **T 682 CZY** aina ya **TOYOTA IST.** Chassis namba **NCP650037706.** Engine namba **1NZB707085.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/URA/RB/975774/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SIMON MICHAEL SHINSHI** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T 665 DVG** aina ya **TATA XENON (RANGI NYEUPE).** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya polisi: **KRI/RB/3098/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SIMON MICHAEL SHINSHI** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T 114 DNJ** aina ya **SUBARU- FORESTER (RANGI YA SILVER).** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya polisi **KRI/RB/3098/2023.**

---

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya DODOMA MJINI**
**Wilaya ya DODOMA**
**Kituo cha CHAMWINO Mkoa DODOMA**
**Shauri la Madai/Ndoa Na. 34/2023**
**JINA LA MDAI............OSCAR SAMSON**
**JINA LA MDAIWA............ATUGANILE MBELE**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakaka za Mwanzo)**

**KWA; ATUGANILE MBELE**
**Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba**
**MADAI YA TALAKA**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 01/09/2023 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta Shahidi/Mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO** kama hautohudhuria siku ilitajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 01/06/2023

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**LILILOKO DODOMA**
**MAOMBI NA. 226 YA 2022**
**TERESIA ANDERSON .........MDAI**
**VERSUS**
**FRANCIS COSMAS ...............MDAIWA 1**
**ELISANTE CHARLES ............. MDAIWA 2**

**KWA:**
**FRANCIS COSMAS**
**POPOTE ULIPO.**
**YAH: KUITWA SHAURINI**
Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 07.06. 2023 saa 3:00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.
**ANGALIZO:** kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na lakiri /Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 14 ya mwezi wa APRILI, 2023.

---

**FOMU MIRATHI - 2**

**YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**

**Usimamizi wa mirathi Na. 802/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU TABU RASHID MRUMBI**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA RAHYM AMINEL TONNY**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 26 Mwezi 06 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 30 Mwezi 05 Mwaka 2023.

HAKIMU

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo Wilaya ya MOROGORO**
**Kituo cha MJINI**
**Mkoa MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi Na. 47/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU MWANAHAWA ABDALLAH WA M/SONGO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA MOSHI MASHAKA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 19 Mwezi 06 mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia:** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa

- Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia *Futa isiyohusika

Imetolewa leo tarehe 05 mwezi 06 mwaka 2023

---

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**ABDULIKADRI SALUM ABDALLAH** anatangaza kupotea kwa hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE241463** iliyotolewa Makao Makuu ya Uhamiaji mnamo tarehe 18/11/2019. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/KIL/RB/192153/2023.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo KIHONDA**
**Wilaya ya MOROGORO**
**Mkoa wa MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi Na. 29/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU BAKARI RASHIDI WA KIHONDA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA ZENA BAKARI**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe **09** Mwezi **06** mwaka **2023** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia:** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa

- Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia *Futa isiyohusika

Imetolewa leo tarehe 31 mwezi 05 mwaka 2023

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA**
**Kituo cha MAKOLE Mkoa DODOMA**
**Shauri la Madai/Ndoa Na.36/2023**
**Jina la Mdai SIKOTI CO. LTD**
**Jina la Mdaiwa CHICO DODOMA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa CHICO DODOMA**
**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake ya 45,912,840/-**
Hivyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe **19** Mwezi **06** Mwaka **2023** Saa **08:00** asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wake na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe **05** Mwezi **06** Mwaka **2023.**

.............................................
**HAKIMU**

---


**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0677020701**
**E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,**
**WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Bilioni 63/- kujenga shule mpya za sekondari nchini

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

SERIKALI imetenga Sh.bilioni 63 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya za sekondari katika kila halmashauri nchini.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Deogratius Ndejembi, alibainisha hayo bungeni jana alipojibu swali la nyongeza la Mbunge wa Singida Mjini (CCM), Mussa Sima.

Mbunge huyo alisema kuna tatizo lililotokea katika Shule ya Sekondari Utemini wilayani Singida na kulazimika kuwahamisha wanafunzi kwenda shule nyingine kutokana na miundombinu kutokuwa rafiki na serikali iliahidi kupeleka fedha kujenga shule hiyo.

Alihoji lini fedha zitaelekwa ili kuboresha na kuongeza miundombinu na samani za shule hiyo.

Akijibu swali hilo, Ndejembi alisema hivi karibuni halmashauri zitapatiwa kila mmoja Sh.milioni 570 ili kuanza ujenzi wa shule za sekondari hizo mpya.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Rungwe (CCM), Anton Mwantona, alihoji lini Shule ya Sekondari Kayuki itafanyiwa ukarabati kama alivyoagiza na Waziri Mkuu.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Ndejembi alisema taratibu za kutekeleza agizo lililotolewa na Waziri Mkuu la kukarabati katika shule hiyo zinaendelea na halmashauri imekamilisha BOQ kwa ajili ya ukarabati wa Shule ya Sekondari Kayuki na Sh. milioni 776 zinahitajika.

"Utaratibu wa kupata fedha kwa ajili ya kukarabati shule hiyo unaendelea ambapo ukarabati mdogo katika hosteli na jengo la utawala umefanyika kwa Sh. milioni 17.4," alisema.

Naibu Waziri alisema serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kukarabati shule hiyo kama alivyoelekeza Waziri Mkuu.



Mwanafunzi wa mwaka wa pili katika Chuo Kikuu cha Mt. Joseph cha jijini Dar es Salaam, Steven Makunga (katikati), akifafanua jambo chuoni hapo jana kuhusu satellite iliyobuniwa na wanafunzi wa chuo hicho wakisaidiana na mhadhiri wao inayotarajiwa kurushwa angani mwishoni mwa mwaka huu. Kushoto ni mbunifu mwenza wa satelite hiyo, Doris Ndaki na mwanafunzi aliyeshiriki, David Seng'enge. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Zitto alia na umaskini unaowaandama wananchi

**Na Julieth Mkireri,**
KAHAMA

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema kitaendelea kushawishi sera mbadala za kuondoa watu katika umaskini ikiwamo kuhakikisha kunakuwa na utaratibu mzuri wa hifadhi ya jamii, hasa kuwa na bima ya afya kwa wote.

Kimesema haikubaliki kuona asilimia 61 ya watu maskini nchini wako mikoa ya magharibi na Kanda ya Ziwa na asilimia 33 ya watu wote maskini nchini wako mikoa ya Geita, Kagera, Simiyu na Mwanza.

Akizungumza katika mkutano uliofanyika mjini Kahama juzi, kiongozi wa chama hicho Zitto Kabwe, alisema wanahitaji uchumi wa Tanzania ukue kwa kasi ya wastani wa asilimia nane kwa mwaka.

Zitto alisema kwa miaka miaka 10 mfululizo, kasi ya umaskini isipungue asilimia sita. Alisema kwa miaka 10 ya mwanzo, kilimo kinapaswa kuwa sekta kuu ya kuchochea ukuaji isiwe chini ya asilimia 6 hadi 8 kwa hiyo miaka 10 mfululizo kwa kufanya hivi tutafuta umaskini nchini.

Zitto alisema ipo haja kurudisha Tume ya Mipango ili kuongoza mwelekeo huo mpya wa kisera, akisitiza siyo sawa miaka 60 baada ya Uhuru karibu nusu ya watu wanaishi chini ya mstari wa umaskini.

"Tunawaahidi kuwa katika jitihada zetu za kuwaunganisha Watanzania kujenga taifa la wote, maslahi ya wote, tutaendelea kuishughulikia masuala ya umaskini wa watu wetu," alisema.

Mwenyekiti wa Chama hicho, Juma Duni Haji, alisema serikali inatakiwa kutoa mikopo na teknolojia rafiki itakayosaidia kugundua, kuchimba na kuchenjua dhahabu kwa kuwa bila teknolojia hakuna thamani.

Duni pia alisema halmashauri zinatakiwa kuwakingia kifua wachimbaji wadogo na kuhakikisha haki zao zinapatikana kwa kuwa wao ndio wanaochangia mapato ya ndani na kuongeza mzunguko wa fedha.

"Sisi ACT-Wazalendo tunaitaka pia serikali kuhakikisha kunakuwa na viwanda vya kuzalisha bidhaa za mwisho za dhahabu badala ya kuuza dhahabu ghafi nje ya nchi, ili kuongeza thamani," alisisitiza.

Mwenyekiti huyo alisema kukosekana kwa teknolojia ya kuchenjua dhahabu kunasababisha iuzwe kwa bei nafuu. Pia mikataba ya madini inayotumika sasa haiendi moja kwa moja katika maeneo husika.

# Wanafunzi wa chuo kikuu wabuni satelaiti

**Na Joseph Mwendapole**

WANAFUNZI wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Joseph cha jijini Dar es Salaam kwa kushirikiana na wahadhiri wao, wamebuni satelaiti ambayo hadi kukamilika kwake itagharimu dola za Marekani 250,000.

Wanafunzi hao ni Steven Makunga, David Seng'enge na Doris Ndaki wanaosoma Shahada ya Sayansi ya Kompyuta mwaka wa pili wakisaidiwa na mwalimu wao, Dk. Amani Bura.

Utengenezaji wa satelaiti hiyo umefikia asilimia 50 na inatarajiwa kurushwa angani kuanzia mwishoni mwa mwaka huu au mwanzoni mwa mwaka 2024 ili kutoa taarifa mbalimbali.

Akizungumza na Nipashe ofisini kwake jana, Makamu Mkuu wa chuo hicho, Prof. Eliab Opiyo, alisema mradi huo unatekelezwa na wanafunzi na wahadhiri wa Kitivo cha Uhandisi na Teknolojia chuoni hapo.

Alisema wanatarajia kuipeleka satelaiti hiyo aina ya 3U Cubesat Kilomita 400 angani kuwezesha ukusanyaji wa taarifa kwa ajili ya utafiti katika maeneo mbalimbali kama vile mabadiliko ya tabianchi na mienendo ya wanyamapori.

Prof. Eliab alisema walianzisha mradi huo miaka miwili iliyopita na kazi inayofanyika kwa sasa ni kutengeneza mfano wa satelaiti na kuifanyia majaribio kadhaa na kuongeza kuwa walishaionyesha kwenye maonyesho ya MAKISATU mkoani Dodoma.

Alisema watakapoirusha angani, itawasaidia kupata taarifa mbalimbali kwa taasisi na watafiti wanaotafuta taarifa muhimu.

Alisema kwa sasa mradi huo unafadhiliwa na Chuo Kikuu cha Mtakatifu Joseph ambacho kimekuwa kikigharamia ununuzi wa vifaa. Mazungumzo ya kushirikisha watafiti na watu wengine yanaendelea.

Alisema mazungumzo hayo ni kwa ajili ya kushirikisha watafiti wa vyuo na taasisi za kitafiti za kigeni ili kusaidia kutoa utaalamu na mafunzo zaidi ya kiufundi, vifaa vya satelaiti na huduma ya kuirusha satelaiti hiyo angani.

Steven Makunga, mmoja wa wavumbuzi wa satelaiti hiyo, alisema wamefikia asilimia 50 ya kazi ya kuiunda. Kwa sasa inaweza kutumika kukusanya baadhi ya taarifa.

Alisema chombo hicho kitakuwa msaada mkubwa katika kupata taarifa za hali ya hewa na mawasiliano katika maeneo ambayo hayajafikiwa na huduma hiyo.

Makunga alisema pia itasaidia kutoa taarifa za kilimo kwa wakulima kuhusu mazao ya kupanda na maendeleo ya mazao yao kwa ujumla.

"Satelaiti hii pia inaweza kutusaidia katika elimu kwa kutoa maudhui ya elimu yetu Tanzania katika vijiji na maeneo ambayo hakuna miundombinu ya mtandao na huduma za simu na pia inaweza kurahisisha mawasiliano katika sekta ya afya," alisema Makunga.

Alisema inaweza pia kuwa msaada mkubwa yanapotokea majanga makubwa kama moto na mafuriko kwa kutoa taarifa za dharura kwa watu wanaokwenda maeneo ya uokoaji.

## HABARI MICHEZO

# SIMBA: USAJILI WACHEZAJI WAPYA UTAKUWA GUMZO

**Na Faustine Feliciane,** MBEYA

UONGOZI wa Simba umesisitiza haitafanya usajili wa 'mihemko' na badala yake watafuata mahitaji na mapendekezo yatakayotolewa na benchi lao la ufundi la timu yao ambalo kwa sasa liko chini ya Mbrazil, Roberto Oliviera 'Robertinho', imeelezwa.

Tayari Wekundu wa Msimbazi wametangaza kuachana na winga, Augustine Okrah, raia wa Ghana baada ya Robertinho kuweka wazi hayuko katika mipango yake.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Simba, Salim Abdallah 'Try Again', alisema uongozi unafahamu mahitaji halisi ya klabu yao na wapo makini katika kila hatua ya mchakato huo wa usajili kwa sababu wanahitaji kuongeza nguvu katika kikosi chao.

**"Mchakato wa usajili unaendelea, kama uongozi tupo makini kwa kila hatua ambayo tutaifanya katika kukiboresha kikosi chetu, tunafahamu yapo maneno yanasemwa huko nje kuhusu usajili wetu, hatuna mihemko, tutasajili kwa utaratibu na umakini mkubwa," alisema Try Again.**

Kiongozi huyo alisema tayari Robertinho ameshatoa mapendekezo katika maeneo ambayo anataka yafanyiwe kazi kuelekea msimu ujao.

Aliwataka wanachama na mashabiki wa Simba kuwa watulivu katika kipindi hiki kwa sababu uongozi umebaini ulipokosea na unaahidi watasajili kikosi imara na kitakachowapa furaha.

"Tutahakikisha tunafanya usajili wa kihistoria, tunasema hatutakurupuka, hatutaki kurudia makosa ya nyuma, tunajua nini tunahitaji ili kufikia malengo yetu kuelekea msimu mpya," alisema Try Again.

Taarifa zilizopatikana jijini Dar es Salaam zinasema Simba imeanza kuhusishwa na usajili wa wachezaji wawili wa Al Hilal ya Sudan mmoja akiwa ni mshambuliaji na mwingine ni golikipa anayesakwa kwa ajili ya kuziba pengo la mlinda mlango namba moja, Aishi Manula ambaye atakaa nje kwa muda wa miezi minne akiuguza majeraha ya kufanyiwa upasuaji.

Baada ya mechi ya jana jioni, kikosi cha Simba kitabakia Dar es Salaam kuendelea na mazoezi ya kuwakaribisha Coastal Union katika mechi ya kumaliza msimu wa 2022/2023 itakayochezwa keshokutwa hapa jijini.



Kiungo wa Ihefu, Raphael Daudi (kulia), akipambana kuwania mpira dhidi ya mchezaji wa Geita Gold FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Highland Estates ulioko Mbarali, Mbeya jana. **PICHA: MTANDAO**

# Mpango: Fedha za michezo zisiguswe

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, ameagiza watendaji wanaohusika na michezo kutobadilisha matumizi ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya michezo hapa nchini.

Mpango alisema hayo katika uzinduzi wa mashindano ya UMITASHUMTA kitaifa na kuongeza fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya michezo zifanye kazi iliyokusudiwa na sio vinginevyo.

Aidha aliagiza na kutoa maelekezo mashindano hayo yashirikishe pia watu wenye ulemavu na hilo ni agizo la serikali.

Alisema kila shule ya msingi na sekondari zinatakiwa kuwa na mwalimu mmoja wa michezo ili kutengeneza vipaji



ambavyo vitaleta tija kwa nchi kwa sababu michezo ina ajira na utajiri duniani.

Alisema wataalamu wote wanaohusika na michezo waweke utaratibu wa namna ya ratiba za michezo yote ili kutengeneza vipaji vitakavyosaidia nchi na jamii kwa ujumla.

Alipongeza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kupewa tuzo ya heshima na Baraza la Michezo la Taifa (BMT), kwa kazi kubwa anayofanya katika sekta ya michezo nchini.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Dk. Batilda Burian, mashindano ya mwaka huu yanashirikisha wanamichezo 3,194 ambao wanasimamiwa na walimu 759 huku akieleza wanafamilia ya michezo wamejipanga vyema kuhakikisha yanafanyika kwa ufanisi.

## Norway, Uswisi wasaidia wasanii

**Na Beatrice Shayo**

VIKUNDI nane vinavyojihusisha na sanaa maalimbani hapa nchini vimepata msaada wa Sh. milioni 187.26 kutoka kwa ubalozi wa Norway na Uswisi ili kutimiza ndoto zao, imefahamika.

Akizungumza na jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Bodi ya Nafasi Arts Space, Tony Ndunguru, alisema vikundi vilivyopata msaada huo ni vile vilivyoibuka washindi na lengo la kuwapa fedha ni kuhakikisha wanafikia malengo.

Ndunguru alisema mchakato huo wa kuwapata wanufaika ulifanyika kwa awamu tatu na mfuko huo umekuwa ukiwathamini wasanii huku wadhamini wakitoa masharti mepesi.

Aliongeza mfuko huo hautoi fedha nyingi kwa wasanii lakini wanatoa kiwango cha fedha kinachowasaidia wahusika kutimiza malengo waliyokusudia.

Alieleza taasisi yao ilipokea maombi ya vikundi zaidi ya 100 lakini walioshinda na kupata maada huo ni Fahari Yetu kutoka Iringa, Adea TZ (Mtwara), Victoria Alex John (Tanga), Wifi (Zanzibar), Emedo (Mwanza), Refixit, Scolastica Sultan na Bahati Female Band, vyote vya Dar es Salaam.

## Ufukweni Tanzania kushindana Afrika

**Na Saada Akida**

TIMU ya Soka ya Taifa ya Ufukweni imepata nafasi ya kushiriki michuano ya pili ya Afrika inayotarajia kufanyika kuanzia Juni 23 hadi 30, mwaka huu katika mji wa Hammamt, Tunisia.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Boniface Pasawa, ametaja wachezaji wanaounda kikosi kitakachojiandaa na michuano hiyo ni Shaban Kado kutoka Ihefu SC, Adam Oseja (Huru), Ally Haji Juma (JKU), Sadiki Salim (Green Warriors), Mtoro Nassoro (Msasani Mabingwa), Ismail Adam (KMC FC) na Suleiman Said wa Zimamoto.

Pawasa aliwataja wengine ni Juma Sultan, Jaruph Rajabu (huru), Abdulrahim Seif, Yahya Haji wa Uhamiaji, Goodluck Dickson (Friends Rangers ), Stephano Wallace (Mburahati), Salum Abdillah (Ilala FC) na Samson Baraka wa Tanzania Prisons.

Alisema kikosi kitaingia kambini rasmi Jumapili kwa ajili ya kujiimarisha kuelekea michuano hiyo lakini kinajipanga kucheza mechi mbili za kirafiki.

Naye Makamu wa Rais wa Kamati ya Olimpiki Tanzania (TOC), Henry Tandau, alisema Tanzania imepata nafasi ya kupeleka timu mbili katika michuano hiyo ambayo ni ya ufukweni na riadha.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### KUREJEA DORTMUND

MCHEZAJI wa Manchester City, Ilkay Gundogan, 32, huenda akarejea Borussia Dortmund msimu huu wa joto kwa sababu Barcelona hawana uwezo wa kulipa mshahara wa kiungo huyo wa kati wa Ujerumani ambaye mkataba wake umemalizika. ***(Bild)***

### BARCA, ARSENAL VITANI

BARCELONA wamejaribu kumshawishi, Ilkay Gundogan, kwa kuongeza ofa yao ya mkataba hadi miaka mitatu na kupunguza mshahara, wakati Arsenal wametoa mkataba wa miaka miwili na dau kubwa pia linatarajiwa kutoka kwa klabu ya Saudi Arabia. ***(Sport)***

### MADRID YAMFUATA KANE

DAU la kwanza la Real Madrid kwa Harry Kane, 29, litakuwa la euro milioni 80, lakini Tottenham awali wamemthamini mshambuliaji huyo wa England thamani yake ni euro milioni 120. ***(Sport)***

### SPURS KUANDAA KITITA

KLABU ya Tottenham itamsaidia kocha anayekuja, Ange Postecoglou, kupata fedha za kuchuana na Newcastle United kumwania kumsajili kiungo wa kati wa Leicester City, James Maddison, 26. ***(Mirror)***

### UGARTE ANUKIA PSG

PARIS St-Germain imeishinda Chelsea katika mbio za kumsajili kiungo wa Timu ya Taifa ya Uruguay, Manuel Ugarte, 22 kutoka Sporting Lisbon. ***(L'Equipe)***

### CAICEDO KUTUA CHELSEA

CHELSEA imeelekeza nguvu zake kwa usajili wa kiungo wa Brighton na Timu ya Taifa Ecuador, Moises Caicedo, 21. ***(Standard)***

### LAVIA ATAJWA CHELSEA

CHELSEA pia imefufua nia yao ya kumnunua kiungo wa Southampton na Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Romeo Lavia, 19. ***(Express)***

### ALLISTER SAFI LIVERPOOL

ALEXIS Mac Allister, 24, atajiunga na Liverpool kutoka Brighton, akifanyiwa uchunguzi wa kimatibabu, huku kiungo huyo wa kati wa Argentina akisadikiwa amekubali mkataba wa miaka mitano. ***(Standard)***

### ATLETICO AMTAKA ZAHA

KLABU ya Atletico Madrid imeulizia kuhusu uwezekano wa kumnunua, Wilfred Zaha. Mshambuliaji huyo wa Ivory Coast mwenye umri wa miaka 30, atakuwa mchezaji huru iwapo ataamua kutokubali mkataba mpya na Crystal Palace. ***(Mail)***

### LIVERPOOL KUMNG'OA KESSIE

LIVERPOOL iko tayari kuilipa Barcelona euro milioni 35 ili kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Franck Kessie, 26. ***(Sport)***

### SPURS YAMWINDA PICKFORD

KLABU ya Tottenham Hotspur imewasiliana na Everton kuhusu uwezekano wa kumnunua mlinda mlango wa England, Jordan Pickford, katika msimu wa joto lakini huenda ikarudishwa nyuma na bei ya mchezaji huyo ambaye bado ana mkataba hadi mwaka 2027. ***(Football transfer)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# LIONEL MESSI ANATAKA KURUDI BARCELONA

**PARIS,** Ufaransa

**Baba na wakala wa mshambuliaji huyo wafunguka na kusema hatima yake...**

BABA mzazi na wakala wa Lionel Messi, Jorge Mendes, amesema mtoto wake angependa kurejea Barcelona msimu huu wa joto.

**Nahodha huyo wa Argentina anafikiria ofa baada ya kuondoka Paris Saint-Germain kama mchezaji huru baada ya misimu miwili na mabingwa hao wa Ufaransa.**

Licha ya kunaswa na kamera akiingia nyumbani kwa Rais wa Barcelona, Joan Laporta, Jumatatu asubuhi, Jorge Messi, alikanusha mkutano huo lakini aliwaambia waandishi wa habari: "Bila shaka, Messi angependa kurudi Barcelona. Ningependa pia. Tutaona."

Barca wanatarajia kupata kibali kutoka Ligi Kuu Hispania, LaLiga, wiki hii kuhusu mipango yao ya kifedha ili kuanza biashara yao ya uhamisho, ambayo itajumuisha kusajiliwa tena kwa Messi.

Alipoulizwa kama alizungumza na Laporta kuhusu jinsi Barca wangeweza kufadhili kurejea kwa Messi, Mendes alisema: "Tulizungumza juzi, lakini hakuna kitu halisi."

Kocha wa Barca, Xavi Hernandez, alisema Messi atafanya uamuzi kuhusu klabu yake ya baadaye wiki hii na imeelezwa "milango iko wazi" kurejea Barca.

Fowadi huyo wa Argentina amechangia mabao 21 na pasi 20 za magoli kwa PSG katika mashindano yote msimu huu.

ESPN iliripoti mnamo Aprili, mwaka huu Messi anafikiria ofa kubwa kutoka kwa timu ya Saudi Arabia Al Hilal, ingawa wakala wake alikanusha ripoti hizo.

Timu ya Ligi Kuu Marekani, Miami CF pia inavutiwa na saini yake.

Messi alikaa Barca kwa miaka 21 na kuisaidia klabu hiyo kushinda mataji 35, lakini aliondoka na kujiunga na PSG Agosti, mwaka 2021 kutokana na matatizo ya kifedha ya klabu hiyo.



# KANE KUMRITHI BENZEMA MADRID

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid inamwona, Harry Kane kama chaguo bora zaidi la kuchukua nafasi ya Karim Benzema, vyanzo vimeiambia ESPN, lakini klabu hiyo inaangalia wachezaji wengine kwa sababu inafahamu kumsajili mshambuliaji huyo kutoka Tottenham Hotspur haitakuwa kazi rahisi.

Nahodha huyo wa England, ambaye amefunga mabao 32 msimu huu, ana wasifu sahihi wa kuichezea Madrid, vyanzo vimesema, lakini kuna maswali juu ya umri, ada yake ya uhamisho na kusita kwa Spurs kumruhusu mchezaji wao mahiri kuondoka.

Madrid walikuwa wamepanga kumsajili mshambuliaji kama vile Joselu wa Espanyol ili kuchukua nafasi ya Benzema na kusubiri hadi majira ya joto yajayo kabla ya kufanya uwekezaji mkubwa mbeleni.

Vyanzo vya klabu vimesita kusema wazi kuhusu nia ya kutaka kumsajili Erling Haaland au Kylian Mbappe, lakini baadhi yao wako tayari kukiri mpango wa kumnunua mmoja kati ya hao wawili ulikuwa umepangwa kufanyika mwaka 2024, wakati muda wa Benzema pale Madrid ungekaribia kumalizika.

Uamuzi wa mshtuko wa Benzema kuondoka Madrid mwezi huu, kukubali ofa kutoka kwa Al Ittihad ya Saudi Arabia sasa umeilazimu klabu hiyo kubadili mipango yao, ili kuhakikisha inapata mshambuliaji bora kwa ajili ya msimu ujao.

Madrid inakaribia kukamilisha usajili wa Joselu kuchukua nafasi ya Mariano lakini sasa watahitaji kumtafuta mchezaji namba 9 ambaye anaweza kuziba pengo la Benzema ambaye amefunga mabao 31 katika michuano yote msimu huu.

Shida ambayo klabu inakabiliana nayo ni kuna chaguzi chache sokoni huku Haaland na Mbappe wakisalia Manchester City na Paris Saint-Germain kwa angalau msimu mwingine.

Hata hivyo, pia kuna mashaka ndani ya klabu kuhusu uwezekano wa kusajiliwa kwa fowadi huyo wa Ligi Kuu England.

Kane atafikisha umri wa miaka 30 mwezi ujao, na sera ya hivi majuzi ya uhamisho ya Madrid imewafanya wajikite katika kusajili vipaji vijavyo kama Vinicius Junior, Rodrygo, Eduardo Camavinga na Aurelien Tchouameni.

# De Bruyne aihofia Inter

**MANCHESTER,** England

KEVIN De Bruyne haamini kama Manchester City inapewa nafasi kubwa ya kuifunga Inter Milan katika mechi ya fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na kupata ushindi wanaouhitaji kukamilisha mataji matatu.

City wana nia kubwa ya kuishinda timu hiyo ya Ligi Kuu Italia (Serie A), hapo Jumamosi mjini Istanbul na kuwa klabu ya kwanza ya England kushinda mataji yote matatu makubwa katika msimu mmoja tangu Manchester United ilipofanya hivyo mwaka 1999.

Jumamosi walitwaa taji FA huku tayari wakiwa wameshinda Kombe la Ligi Kuu, huku mabao ya Ilkay Gundogan yakiwasaidia vijana hao wa Pep Guardiola kushinda mabao 2-1 dhidi ya United mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Wembley.

Lakini baada ya ushindi wa fainali ya kombe hilo, De Bruyne alikiri jinsi yeye na wachezaji wenzake walikuwa karibu na mafanikio ya ajabu, lakini alisita kusema walikuwa wanapewa nafasi kubwa kuishinda Inter.

"Kuna imani hiyo, lakini siwezi kusema kwa uhakika kabisa," alisema.

"Tunajua sasa. Nataka kushinda Ligi ya Mabingwa na ninataka kushinda mataji matatu lakini tulikuwa tukijiandaa kushinda mchezo dhidi ya United.

"Tulistahili kushinda. Nina furaha na fahari sana. Tunapaswa kufurahia na tunatumaini tunaweza kufanya vyema tuwezavyo.

"Inter ni timu nzuri sana. Fainali ni 50-50. Daima ni vigumu. Lazima udhibiti nyakati hizi. Kutakuwa na wakati ambapo ni ngumu lakini katika dakika kubwa tunajaribu kufanya kazi yetu.





# Pulisic: Nilikuwa na msimu mgumu

**CALIFORNIA,** Marekani

KIUNGO wa kati wa Timu ya Taifa ya Marekani, Christian Pulisic, amekiri msimu wake wa 2022-23 akiwa na Chelsea ulikuwa "mgumu sana."

Pulisic alizungumza na waandishi wa habari kutoka Carson, California, ambapo alisema ana nia ya kurejea "kuwa mchezaji ninayejiamini. Najua naweza kuwa hivyo."

Kwa mujibu wa takwimu, msimu uliomalizika ulikuwa mgumu zaidi katika kipindi cha Pulisic akiwa na The Blues hao.

Alirekodi dakika 813 pekee kwenye Ligi Kuu England, alama yake ya chini zaidi tangu alipokuwa Borussia Dortmund msimu wa 2015-16.

Hata kwa kila dakika 90, miguso ya Pulisic (45.98), mabao (0.1), mabao yaliyotarajiwa (0.14), mashuti (1.75) na mashuti yaliyolenga lengo (asilimia 27), yote yalikuwa chini zaidi kuliko msimu wa kwanza akiwa hapo Chelsea.

"Umekuwa msimu mgumu sana kwangu binafsi na kwa timu yetu bila shaka katika ngazi ya klabu," alisema Pulisic.

"Kwa hiyo kwangu mimi ni kuingia hapa na kuanza upya na kuwa sehemu ya timu ambayo natumaini inaweza kutoka na kushinda baadhi ya michezo.

Kupungua kwa nafasi ya Pulisic akiwa na Chelsea, pamoja na wingi wa wachezaji kwenye orodha ya The Blues walioletwa tangu mmiliki mpya, Todd Boehly kuwasili, kumetoa hisia atabadilisha klabu wakati wa majira ya joto.

Vyanzo viliiambia ESPN Juventus ndio mahali pengine kwenda kwa kijana huyo mwenye umri wa miaka 24.

## Pazia Ligi Kuu Z'bar kufungwa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BINGWA wa Ligi Kuu Zanzibar atajulikana katika mechi za kumaliza msimu wa mwaka 2022/2023 zinazotarajiwa kuchezwa leo katika viwanja mbalimbali visiwani hapa.

Vinara KMKM wenye pointi 66 wanapewa nafasi kubwa ya kutwaa taji hilo lakini wakipewa presha na KVZ yenye pointi 65 ambayo pia inaamini inaweza kuibuka na kombe hilo.

KMKM leo itashuka dimbani dhidi ya Chipukizi FC ya Pemba mchezo utakaopigwa kwenye Uwanja wa Mau B, wakati wapinzani wao watamana na Dulla Boys ambayo tayari imeshashuka daraja katika dimba la Mau A.

Kocha Msaidizi wa KMKM, Ame Msimu, alisema anafahamu mchezo wa mwisho watakutana na ushindani kwa sababu Chipukizi ni timu ngumu lakini wamejipanga kupambana ili kushinda na kutwaa ubingwa.

Naye Kocha Msaidizi wa KVZ, Ali Khalid, aliliambia gazeti hili wamejiandaa vyema kupata alama tatu bila kuangalia wao KMKM atashinda matokeo ya aina gani.

"Lazima tucheze kwa kusaka alama tatu, ndani ya dakika 90 ndio atajulikana nani bingwa, tumejiandaa vizuri na tuaenda kucheza bila kuangalia timu tunayocheza nayo tayari imeshuka daraja, katika soka lolote linawezekana," alisema kocha huyo.

## Morrison arejesha furaha, Mbeya City, KMC hesabu bado

INATOKA UKURASA 24

ziliwakuta wachezaji, Moloko na Hassan Nassoro wa Mbeya City kutolewa nje kwa kuonyeshwa kadi nyekundu na mwamuzi, Tatu Malogo, kutoka Tanga.

Katika mechi nyingine KMC ilijiweka katika wakati mgumu kwa kucheza mechi za mchujo, baada ya kuchapwa bao 1-0 na wenyeji Prisons, mechi ikichezwa mjini Sumbawanga, mkoani Rukwa.

Bao lililofungwa na Edwin Balua limeifanya Prisons kufikisha pointi 37 na kupanda hadi nafasi ya saba, huku KMC ikisalia katika nafasi ya 14 na pointi zake 29 huku Mtibwa Sugar iliyowafunga Kagera Sugar mabao 3-0 yameifanya kupanda hadi katika nafasi ya 11.

Mabao ya Mtibwa Sugar yalifungwa na Omari Selemani, Martin Ilamfya na Vitalis Mayanga wakati Ihefu SC, ikiwa nyumbani, Highland Estates, Mbarali, Mbeya imeichapa Geita Gold mabao 3-1 na Singida Big Stars ikitandika Ruvu Shooting iliyoshuka daraja mabao 2-1, mechi ikichezwa kwenye Uwanja wa Liti, Singida kwa mabao ya Bruno Gomes na Meddie Kagere na Valentino Mashaka akiifungia Ruvu Shooting.

Kwenye Uwanja wa Mkwakwani Tanga, Azam FC ilipata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Coastal Union na kujichimbia katika nafasi ya tatu ikifikisha pointi 56.

# UWANJA WA MKAPA SASA MICHEZO YA KIMATAIFA TU

**Na Jenifer Gilla,** DODOMA

WIZARA ya Utamaduni, Sanaa na Michezo imesema ipo mbioni kuanza marekebisho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam ili kuurudishia hadhi yake.

**Waziri wa wizara hiyo, Dk. Pindi Chana, aliliambia Bunge, jijini hapa jana wakati anahitimisha bajeti ya o alisema ujenzi utaanza mara moja baada ya kumalizika kwa mechi kati Tanzania (Taifa Stars) dhidi ya Niger.**

Alisema uwanja huo sasa utatumika katika mechi za kimataifa na michezo mingine itacheza kwenye viwanja mbadala ili kuupunguzia mzigo na kuepusha kuharibika.

Aliongeza serikali pia itajenga viwanja vya mpira vyenye hadhi za kimataifa viwili katika mkoa wa Dodoma na Arusha ikiwa ni maandalizi ya kuandaa fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) zitakazofanyika mwaka 2027.

"Ili ukidhi AFCON unahitaji viwanja nane vya kimataifa, lakini kwa kuwa tumeomba pamoja na Kenya na Uganda tukichanganya vitatimia, wanatarajiwa kuja wakaguzi kutoka CAF (Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika) kuona namna gani tumekidhi vigezo," alisema Chana.

Aliongeza wanaipa kipaumbele suala la ushiriki wa michezo katika shule za msingi na sekondari na kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kila shule inatakiwa kuwa na kiwanja cha michezo ili watoto wapate fursa ya kushiriki vyema.

Pia Chama alisema wizara yake imeunda kamati ya kuratibu vazi la taifa ili kuharakisha mchakato huo na imeshawapa maagizo ya kuharakisha vazi hilo linapatikana na hivi karibuni watawasilisha ripoti maalum kuhusiana na maoni walipokea kutoka kwa wadau.

Alisema pia wana mpango wa kushirikiana na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), ili kuweka utaratibu wa kutoa vibali kwa wadau wanaotaka kuendesha mashindano ya Ndondo kwa sababu michuano hiyo ni moja ya sehemu ya inayozalisha vipaji.

Akijibu baadhi ya hoja za wabunge , Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma 'Mwana FA' alisema wizara hiyo imeshaanza kufanya mawasiliano na Wizara za Fedha, Nishati na Madini ili kukamilisha ujenzi wa viwanja vikubwa viwili vitakavyojengwa Arusha na Dodoma huku pia wakijipanga kufanya ukarabati viwanja vilivyoharibika.



Mchezaji wa Mtibwa Sugar, Vitalis Mayanga (kulia), akimzuia nyota wa Kagera Sugar kupata mpira katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Manungu Complex, Morogoro jana. Mtibwa Sugar ilishinda mabao 3-0. **PICHA: MTANDAO**

## *Wabunge wacharuka bajeti ndogo Michezo*

INATOKA UKURASA 24

Alisema wizara hiyo ilipaswa kutengewa fungu kubwa kwa kuwa ndiyo inayolibeba taifa na kuwatambulisha Watanzania na ina mambo mengi na makubwa ya kufanya.

Alisema katika michezo kunahitajika kujengwa viwanja vizuri. Pia kupelekwa wataalamu wa michezo shuleni ili kuwafundisha watoto michezo na kuibua vipaji.

Mbunge wa Makete, Festo Sanga, aliitaka wizara hiyo kutafuta wadau kama vile kampuni zinazomiliki migodi na za michezo ya kubahatisha ili zisaidie kujenga viwanja vya michezo kwa kuwa fungu linalooombwa, hakuna cha maana kitakachofanyika.

Pia aliinyoshea kidole wizara kwa makato makubwa katika mapato ya viwanja toka kwa timu za mpira miguu nchini kwa kuwa zinatumia fedha nyingi kujiandaa kwa mashindano husika.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, akichangia hoja, aliitaka ni moja ya wizara zilizopewa kipaumbele kwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan ni mwanamichezo na amekuwa akizishika mkono timu za michezo ili zifanye vizuri.

Alisema matarajio ya serikali ni kuwa yale ambayo yanaweza kufanywa kwa ufanisi na sekta binafsi yasitengewe fungu katika bajeti kutokana na kukua kwa mahitaji katika nchi. Ndiyo sababu fungu la wizara hiyo kuonekana dogo.

"Mheshimiwa Mwenyetiki, kwa kweli tutakuwa hatuitendei haki sekta binafsi tukitaka hata magoli ya uwanja kwamba lazima yatengewe bajeti kutoka Mfuko Mkuu (Hazina), kuna vitu vingi ambavyo tunaweza tukavifanya ambavyo sekta binafsi haiwezi ikafanya.

"Katika haya ya michezo, tuna fursa nyingi ambazo sekta binafsi inaweza kufanya na kuifanya bajeti hii kuwa kubwa," alisema.

# Michezo

Jumatano Juni 7, 2023

Nipashe



Messi anataka kurudi Barca UKURASA 21



Wachezaji wa Yanga, Bernard Morrison (kushoto) na mshambuliaji, Clement Mzize, wakishangilia baada ya kufunga bao katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Sokoine jijini Mbeya jana. Timu hizo zilitoka sare ya mabao 3-3. **PICHA: MTANDAO**

# Wabunge wacharuka bajeti ndogo Michezo

**Na Jenifer Gilla,** DODOMA

●●● Watunga sheria walia na makato ya kinyonyaji. Migodi ishirikishwe utekelezaji wa miradi. Kampuni michezo ya kubahatisha zaitwa. Viwanja vingi vya kisasa, walimu wa michezo shuleni...

WAZIRI wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Pindi Chana, ameahidi serikali itafanyia kazi hoja za wabunge ikiwamo ya kuongeza bajeti kwa ajili ya wizara hiyo kwa mwaka ujao wa fedha.

**Ni ahadi aliyoitoa bungeni jijini hapa jana alipohitimisha hoja yake ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka 2023/24 ambayo wabunge waliitaja ni ndogo na kuitaka serikali iangalie namna ya kuiongeza.**

Wizara hiyo imepanga kukusanya na kutumia Sh. bilioni 35.44 kwa mwaka ujao wa fedha, kukiwa na ongezeko kidogo kulinganisha na Sh. bilioni 34.42 ilizoidhinishiwa kwa ajili ya mwaka huu wa fedha.

Mbunge wa Morogoro Kusini, Hamisi Taletale, maarufu Babu Tale, alisema ni aibu kuona wizara inayoleta sifa kubwa kwa nchi inakuwa na bajeti ndogo kuliko zote.

Aliitaka serikali kutafuta njia ya kuangalia namna itakavyoiongeza fedha wizara hiyo ikiwamo kuihamishia michezo ya kubahatisha katika wizara hiyo toka Wizara ya Fedha na Mipango.

"Leo kuna wizara zina zaidi ya Sh. trilioni tatu. Wizara ya Michezo ina Sh. bilioni 35. Ni udhalilishaji huu. Ni aibu kwa wizara na ni aibu kwa serikali ya awamu ya sita ya Mama Samia, kama tunataka tumsaidie Rais Samia, ni lazima tuangalie tunakwama wapi," alisema Taletale.

Mbunge wa Mchinga, Salma Kikwete, pia alikosoa wizara hiyo kuwa na fungu dogo, akisisitiza ina idara nyeti ya utamaduni ambayo ndiyo maisha ya kila siku ya mwanadamu. Alisema fungu lililoombwa haliwezi kuifikisha popote.

INAENDELEA UKURASA 23

## Morrison arejesha shangwe, Mbeya City, KMC, Mtibwa hesabu bado

**Adam Fungamwango na Faustine Feliciane,** MBEYA

GOLI la dakika za majeruhi lililofungwa na Bernard Morrison liliwaweka wenyeji Mbeya City katika wakati mgumu wa kubakia kwenye Ligi Kuu Bara baada ya kulazimishwa sare ya mabao 3-3 dhidi ya Yanga katika mchezo uliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Sokoine jijini hapa jana.

Mbeya City watapaswa kujilaumu wenyewe kwa kutolinda magoli yao matatu ya utangulizi na kuwaruhusu Yanga kipindi cha pili kuwashambulia mfululizo.

Matokeo ya jana yamewafanya Mbeya City kufikisha pointi 31 na kuweka rehani katika majaliwa yao.

Mbeya City walikuwa wa kwanza kupata magoli katika dakika ya tatu lililofungwa na George Sangoja na mengine mawili kupitia, Richardson Ng'odya aliyefunga dakika ya 23 na 54 lakini iliruhusu Yanga iliyowaanzisha wachezaji wengi wa kikosi cha pili kusawazisha.

Dakika ya 65 Morison aliiandikia Yanga bao la kwanza kwa penalti iliyotokana na beki wa Mbeya City kumwangusha Jesus Moloko katika eneo la hatari na dakika ya 70, Salum Abubakary 'Sure Boy' alifunga goli la pili.

Mbeya City walionekana kujichanganya kwenye kuokoa mipira mingi na kuwapa nafasi Yanga kupanga mashambulizi huku mashabiki wao wakiamini wataondoka na ushindi, Morrison alifuta matumaini kwa kupachika wavuni bao tatu ambalo liliamsha shangwe kwa mashabiki wao.

Hata hivyo vurugu za dakika 74

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >